

YEHOVA-YIRE ³



Tuinamishe vichwa vyetu dakika moja kwa maombi.

Naye akapaita mahali hapo Yehova-yire: kama panavyoonekana katika mlima wa BWANA hata leo.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru usiku wa leo kuwa tumepata majaliwa haya ya kukutanika pamoja katika Jina la Bwana Yesu, kumwabudu katika Roho wa kufufuka Kwake. Nasi tuna shukrani tele Kwako, kwa yale ambayo umekwisha tufanyia, kwa kujitambulisha Mwenyewe kwa Neno miongoni mwetu, na kwa ufufuo. Na matumaini yetu yameinuliwa juu sana, Bwana, kwa kuwa tunajua ya kwamba—ya kwamba Mungu tunayemtumikia si mungu fulani wa kihistoria, bali ni Mungu wa wakati uliopo, Yule aliyefufuka kutoka kwa wafu, na amethibitisha kuwa ni Mungu yule aliyekuwa pamoja na Musa, na pamoja na Ibrahimu, na mitume wote, na angali ni Mungu yeye yule. Ndipo ninii yetu... Tunajiunga na Eddie Perronet, kama alivyosema, “Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu kingine pungufu ila Damu ya Yesu na haki Yake.” Kwa hiyo, tunakushukuru kwa maliwazo haya makuu na faraja tuliyo nayo.

³ Baba, usiku wa leo, kama kuna mmoja hapa miongoni mwetu, usiku wa leo, ambaye hana tumaini hili kuu, jalia hii iwe ndiyo ile saa ambayo hiyo Kweli kuu ya Milele itafunuliwa kwao, Baba, kusudi wajue ya kwamba sababu ya wao kuwa hapa duniani si kuninii tu—kufanya kazi. Na hiyo ni moja ya sababu, bila shaka. Lakini sababu kuu ni kuwa mwana ama binti wa Mungu. Na jalia hilo litimilike, usiku wa leo. Tujalie, Bwana.

⁴ Tubariki sasa tunapokuwa na ushirika kwenye Neno Lako. Neno Lako ndilo ile Kweli. Na jalia Roho Mtakatifu aliye mkuu alichukue Neno la Mungu na kutugawia kadiri tulivyo na haja, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵ Asanteni kwa nafasi ya kurudi tena usiku wa leo, na kusimama tena mbele ya ninyi watu wazuri na Injili hii tukufu. Tumetangaza ya kwamba, sasa, kesho asubuhi ile shule ya Jumapili, ya wachungaji walioungana na wanaoshirikiana wana shule ya Jumapili ya pamoja papa hapa. Nafikiri hilo ni zuri kabisa. Na wengi wao wamechukua viti kutoka makanisani mwao na kuvileta hapa kwa ajili ya watu, na kwa kweli ni jambo zuri la uaminifu kwa hao watu kufanya hivyo.

⁶ Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya hali nzuri ya hewa ambayo ametupa. Walibashiri tungekuwa na matufani na kadhalika, wakati wote. Lakini amezuia tufani, wala

hatujakuwa na shida ndogo kabisa hata moja. Tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

⁷ Na sasa, usiku wa leo tulipewa . . . Tumekuwa tu na ibada za kawaida za kiinjilisti. Na kama wapo wageni wowote miongoni mwetu . . . Hatujasisitiza sana juu ya—ya wenye dhambi kuja kwa Kristo. Nami nilichukua somo Alhamisi iliyopita usiku, na wala bado sijalifikia. Tumekuwa tukizungumza tu juu ya Ibrahimu, wala kamwe hatujalifikia somo hilo bado, la *Yehova-Yire*. Kwa hiyo tunajaribu kulimalizia hilo usiku wa leo. Na tunatumaini ya kwamba Bwana atamwokoa kila mtu asiyeokoka, na kumjaza kila mmoja ambaye hajajazwa na Roho Mtakatifu, usiku wa leo.

⁸ Sasa hebu liwazieni hilo kwa makini sana wakati tukiwa tupo hapa. Na wakati tukiwa—wakati tukizungumza, fungua moyo wako ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kuzungumza nawe ndani yako. Tunafanya nini hapa, hata hivyo? Hebu wazieni tu jambo hilo vizuri. Je! maisha yako yamekuwaje? Upo hapa kwa sababu gani? Je! Mungu . . . Je! uko katika hali ambayo Mungu anaweza kupata yote—yote ambayo kwa sababu hiyo alikuweka hapa, kutoka kwako? Kama sivyo, basi hebu na tulitatie jambo hilo usiku wa leo, enyi marafiki. Ni ninii . . .

⁹ Ni—nina baadhi ya marafiki walio hapa, kutoka kanisani mwangu. Baadhi ya ninii . . . Mmoja wa wadhamini, ninajua, na ndugu wawili ama watatu. Nimetambua tu familia ngeni inayoketi hapa, usiku wa leo, akina Palmer kutoka hapa mahali fulani, wanaendesha gari maili mia kadhaa kila—kila Jumapili ninapohubiri huko Indiana. Na Bw. Welch Evans na familia yake wako hapa mahali fulani. Sijui tu ni wapi. Mimi . . . Leo, nimekuwa nikisoma, karibu siku nzima, na ningeweza kusikia sauti zao huko nje. Nami ni—nilijua walikuwa wapo hapa.

¹⁰ Sasa, kesho, kesho saa nane. [Mtu fulani anasema, “Nane.”—Mh.] Saa nane, kesho, ibada yote kesho alasiri imetolewa kwa ajili ya wagonjwa, kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa. Sasa, watu wengi huiita ibada ya uponyaji. Vema, hatupendi hata kuiita hivyo. Kwa sababu, hebu na tuiite ibada ya imani. Kwa hiyo, kama imani yetu inaweza kufikia kwenye kiwango hicho, baada ya Yeye kujitambulisha miongoni mwetu, na anajua kila kitu kilichoko moyoni mwetu, na ametuthibitishia jambo hilo, unaona, ya kwamba Yeye yu hai, na kulithibitisha kwa Maandiko.

¹¹ Je! mliona jinsi alivyounga mkono kila Neno, kwa Uwepo Wake ulio hai? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Mnaona? Mnaona? Sasa, hilo linaonyesha ya kwamba haiwabidi kuwazia tu kwamba tunajaribu kusema tu jambo fulani ambalo ni kitu fulani cha kubuniwa. Yale ambayo Biblia hii imeahidi, hayo ndiyo Kweli. Unaona? Sasa kila Neno ni kweli.

¹² Sasa, huenda nisiwe na imani ya kutosha kufanya kila Neno Lake litende kazi, bali hakika nisingemzuia mtu yeyote ambaye kweli alikuwa na imani hiyo. Henoko alikuwa na imani ya kutosha, siku moja, kwenda kwenye matembezi ya alasiri pamoja na Mungu, na akaendelea tu kutembea, akaenda juu Nyumbani bila ya kufa. Sasa, nafikiri Kanisa halina budi kufikia hilo, kwenye imani ya Kunyakuliwa. Huenda nisiwe na imani hiyo sasa hivi, bali hakika nisingemzuia mtu fulani ambaye alikuwa na imani hiyo.

¹³ Kwa hiyo, tunatumaini ya kwamba Mungu atatupa imani kuu, na, kesho kwamba hakutakuwako na mtu mnyonge aliyesalia jengoni, wakipitia kwenye maombi. Tutaamini tu jambo hilo. Na sasa kama tutaliamini! Sasa, nimeliona hilo mara nyingi sana!

¹⁴ Nimeona wakati ambapo elfu ishirini na tano, hebu wazieni tu sasa, si elfu mbili mia tano, uponyaji wa ajabu wa watu elfu ishirini na tano ukitukia kwa sala moja: Durban, Afrika Kusini. Walipakia, sijui ni malori mangapi makubwa, ambayo mnaninii... Mawili ya hayo yangejaza kitu hiki chote *hapa* ndani, kuenea kile kilichowekwa mle ndani, lori kubwa la Kiingereza, lenye magurudumu sita na manane, namna hiyo, lori tu baada ya lori, yakiteremka, yakiwa na rungu na viti vya magurudumu, ama vile wanavyoviita viti vya magurudumu, vitu vidogo wanavyobebewa navyo wagonjwa. Na kuwaleta kupitia msituni. Na simba angewafukuza, wangewapandisha juu ya mti. Na baadaye wakiendelea kuja mkutanoni. Na halafu kuona tu, jukwaani, mvulana.

¹⁵ Wa kwanza aliyekuja jukwaani alikuwa—alikuwa ni mwanamke. Naye alikuwa ana alama ya Kiislamu, akiwa na doa jekundu kati ya macho yake. Nami nikamwuliza kama alizungumza Kiingereza. Naye akasema, “Kidogo tu.”

Nami nikasema, “Ninaona wewe ni Mwislamu, Mwislamu.”

Akasema, “Ndiyo.”

¹⁶ Nikasema, “Kwa nini unanijia mimi, nami ni Mkristo? Kwa nini usiende kwa kasisi wako?”

Akasema, “Ninaamini ya kwamba unaweza kunisaidia.”

¹⁷ Ndipo nikasema, “Vema, siwezi kukusaidia, isipokuwa, wewe umwamini Yesu Kristo.”

Naye akasema, “Vema, nimeona ibada hizi.”

¹⁸ Kuwepo tu hapo kwa muda wa siku tatu. Tulikuwa na kama, karibu mia mbili elfu walioketi pale wakati huo, mahali hapo. Kwa hiyo basi walikuwa wamewazingira kwa ua, maana walikuwa na vita vya makabila, pia.

¹⁹ Nami nikasema, “Vema, sasa, inakubidi kumwamini Yesu Kristo.” Kisha nikasema, “Umeshawahi kusoma A—Agano Jipya?”

Akasema, “Nimesoma.”

²⁰ Nikasema, “Ulifikiri nini juu ya Ujumbe ambao ndio kwanza nihubiri, kuhusu Yeye kuwa yeye yule jana, leo, na hata milele?”

Akasema, “Ninauamini.”

²¹ Nami nikasema, “Basi kama Bwana Yesu alikuwa yu hai leo, Yeye tayari amekuponya. Kuhusu kuteswa Kwake, uponyaji tayari umeisha patikana. Lakini inakubidi kuwa na imani. Na kama Yeye angalikuwa hapa, Yeye angalijua wewe ulikuwa ni nani. Angalijua yale umefanya. Angalijua yote kukuhusu wewe. Unaamini hilo?”

Akasema, “Ndiyo, bwana.”

²² Nikasema, “Kama Yeye atafunua hilo, je! unaamini Yeye, basi, angekuwa ni Mwana wa Mungu, na amefufuka kutoka kwa wafu, naye anaishi hapa daima sasa? Roho Wake ndani yangu, na pamoja na hawa Wakristo wengine?”

Akasema, “Ninaamini.”

²³ Nikasema, “Sababu ya wewe kuwa hapa...Mume wako ni mtu mfupi, mnene. Ana masharubu meusi. Majuma mawili yaliyopita, ulikuwa kwa daktari. Hili hapa jina lako.” Nisingeweza kuliandika, nisingeweza kulitamka. Ilinibidi kuendeleza herufi zake. Lilikuwa ni jina la Kiislamu.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

²⁴ Nami nikasema, “Basi, na mume wako alingojea sebuleni. Alikuwa amevaa suti ya kijivu na kofia ya hudhurungi.” Nikasema, “Huyo daktari ni kama alikuwa mtu mrefu, mwembamba, alivaa miwani kubwa yenye fremu za pembe. Alikufanyia uchunguzi wa akina mama, na akagundua kwamba ulikuwa na uvimbe kwenye ovari.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

Nikasema, Je! unamkubali Yesu kama Mwokozi wako?”

Akasema, “Yesu Kristo na awe Mwokozi wangu.”

Aliyefuata alikuwa ni maskini mvulana mwenye makengeza.

²⁵ Nao wangewaacha tu wamishenari waende, walete mmoja ama wawili kutoka kwenye kila kabila. Usingeweza kuwazuilia, hakuna njia kamwe. Kwa hiyo, walikuwa na mamia na mamia ya wanajeshi wakijaribu kuwazuilia, nao wasingeweza kuwazuia.

²⁶ Na kwa hiyo basi huyu maskini, mvulana mwenye makengeza, walimweka jukwaani, umbali kama *huo*.

²⁷ Na huko juu jukwaani, yale mayungiyungi makubwa ya Kala. Ninyi akina dada hapa, mnaopenda maua! Baadhi ya hayo mayungiyungi ya Kala kule yana upana wa inchi kumi na nane; ya kimanjano, meupe, mazuri. Nao walikuwa nayo. Ni ya porini tu. Walikuwa wameweka mashada ya maua pale.

28 Nami nilikuwa nikizungumza. Walimketisha mvulana huyo mdogo pale. Huyo mmishenari alimketisha. Na maskini mtoto huyo alikuwa na makengeza. Alikuwa ndiyo kwanza ale chakula chake cha jioni.

29 Wakati mwingine ninii yao—mlo wao ni wa kuchekesha sana. Alikuwa... Wanachukua mwiba mdogo wa nungu na kuchoma vena za ng'ombe, katika kile wanachokiita ninii—ndoo. Ni kijigunia kidogo, ngozi iliyunganishwa kwa kushonwa, na kuachilia da—damu, damu iliyo joto, itiririkie mle. Kisha wanakamulia maziwa kidogo ndani yake, wanayasuka, inafanya pe—peremende kijiti tamu sana.

Usingependa moja ya hizo, sivyo, mpenzi? La.

30 Basi hilo, lakini, yeye, hizo ndizo alizokuwa akila. Na macho yake madogo yalikuwa na makengeza. Nikasema, “Sasa, mtu yeyote anayeweza kuona, atajua mtoto huyu ana shida gani. Macho yake yana makengeza. Kama ningeweza kumsaidia mtoto huyo mchanga,” nikasema, “bila shaka ningemsaidia. Lakini si—siwezi kumsaidia, si zaidi ya mtu mwingine yeyote yule.” Nikasema, “Kama daktari angaliweza, mbona, kama asingefanya hivyo, basi kungekuwa kuna kitu fulani kibaya sana moyoni mwa daktari huyo, kama angeweza kumsaidia.” Nikasema, “Sidhani wangekuwa na njia yoyote ya kufanya kwenye wakati huu.”

31 Nikasema, “Lakini, sasa, Bwana anaweza kunifunulia kumhusu mtoto huyu mchanga.” Na ndipo, Yeye akasema, “Mtoto huyu, baba na mama yake wote wawili ni wembamba.” Hiyo ilikuwa... Mama alikuwa Mzulu, na kwa kawaida wao ni wanene. Nikasema, “Ndio hawa wameketi papa hapa sasa. Jina lao ni *fulani-na-fulani*.” Kisha nikasema, basi, “Mtoto huyu alizaliwa akiwa na makengeza. Sababu, mama yake... Wanatoka katika... Wanaamini Ukristo, kwa sababu ndani ya nyumba yao ndogo, iliyoezekwa kwa nyasi, imo picha ya Kristo, imetundikwa upande wa kulia wa ukuta.”

32 Ndipo nikasema, “Na mtoto huyo mchanga, mara mama alipomwonyesha mtoto huyu kwa baba yake, alikuwa na makengeza.” Huyo baba na mama wakasimama, kuthibitisha hiyo ilikuwa ni kweli. Nikamwangalia mtoto huyo mchanga tena, macho yake yalikuwa mazima kama yangu.

33 Kwa hiyo nikasema, “Sasa, unaona, Bwana,” nikasema, “sijakuwa futi kumi toka alipo mtoto huyo, mtoto huyo ameponywa.”

Nikampisha tu. Ndipo nikamwita aliyefuata.

34 Ndipo wakati hilo lilipotukia, nilisikia vurugu. Dr. Bosworth na Dr. Ern Baxter, mameneja wangu, katika mkutano huo, walikuwa wakibishana na mtu fulani, nami... wakisababisha vurugu kubwa. Jamaa huyu alikuwa akijaribu kuja jukwaani, ama akijaribu kupanda pale. Na palikuwa na madaktari kadhaa,

madaktari wa tiba walioketi pale. Kwa hiyo daktari huyu wa tiba, a—alisema, alikuwa akizungumza. Akasema, “Ninataka kuzungumza naye juu ya mtoto yule mchanga.”

Nikageuka, nikasema, “Kuna nini, daktari?”

Akasema, “Ulijuaje nilikuwa daktari?”

³⁵ Nami nikasema, “Wewe ni daktari. Wewe ni... Ulilelewa, huko Uingereza. Wewe ni daktari Mwingereza.” Kisha nikamwambia mahali alikoenda shuleni.

³⁶ Akasema, “Sasa, Bw. Branham, ninaweza kuelewa mahali ambapo telepathia ya akili inge—ingeweza kusoma akili zangu.”

Nikasema, “Mimi sisomi akili yako, daktari.”

³⁷ Naye akasema, “Lakini kile nisichoweza kuelewa...” Kasema, “Ninaamini ya kwamba Mungu yupo. Pia ninajua ya kwamba yungiyungi lile haliwezi kuishi pale bila ya Mungu,” kasema, “maana lina uhai ndani yake.” Akasema, “Lakini je! Yeye anaweza kushikika? Nilimweka mtoto yule jukwaani. Nikamchunguza. Macho yake yalikuwa yana makengeza kabisa pale. Na huyu hapa mtoto huyo sasa akiwa ana macho ya kawaida. Ni kitu gani kilifanya jambo hilo, Bw. Branham?”

Nikasema, “Yesu Kristo.”

³⁸ Naye akasema, akasema, “Vema, sasa angalia,” akasema, “Mimi ninamwamini Mungu.” Akasema, “Lakini ninataka kukuuliza swali, kama mhudumu sasa. Je! ulimhiponzi yule mtoto?”

³⁹ Nikasema, “Bwana, na hivi unataka kusema Shi—Shirika la Tiba la Uingereza lilikupa leseni ya kufanya kazi ya udaktari, nawe hujui kuhusu hiponzi zaidi ya hivyo? Kama hiponzi itayanyosha macho ya watoto wachanga, unapaswa kuwa ukitumia hiponzi.” Mnaona?

Naye akasema, “Vema, niambie ni kitu gani kilichofanya jambo hilo.”

Nikasema, “Yesu Kristo.”

Akasema, “Angalia,” kasema, “Ninaamini. Nilisema Mungu yuko katika yungiyungi lile.”

⁴⁰ Naye Bw. Bosworth akasema, “Sasa, utasababisha ghasia hapa.” Maana, walikuwa na ubaguzi, pia, kule, unajua.

⁴¹ Na kwa hiyo nikasema, “Utaninii...” Halafu, vita vya kikabila. Nikasema, “Utasababisha ghasia sasa. Usifanye hivyo.” Nikasema, “Unachukua wakati mwingi kupita kiasi kwa mtoto yule.”

⁴² Halafu nikasema, “Hivi ndivyo inavyokupasa kufanya. Mtoto huyo alikuwa amesimama pale. Ulimweka jukwaani. Ni imani yake mwenyewe, na imani ya mama yake, kwa kumwambia hivyo, iliyoimponya mtoto huyu. Macho yake yalikuwa na makengeza pale, hakunigusa kamwe, wala

hakuwa karibu na mimi, ama chochote kile. Hata sikufanya zaidi ya kumwanguka na kumwona huyo mtoto, nikaangalia kusanyiko tena, nikaona ono, nikasema ilikuwa ni kitu gani, kisha nikaangalia nyuma, macho ya huyo mtoto yalikuwa yamenyoka.”

⁴³ Ndipo akaenda chini ya mikrofoni hiyo kubwa ya utando. Akasema, “Ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu.” Mnaona?

⁴⁴ Nilipokuwa nikiondoka Durban, aliruka juu ya ua, ambapo watu wengi, karibu watu kumi, ishirini elfu walikuwa huko nje kutuaga, na... Ama, kuondoka (si Durban, nasikitika) Johannesburg. Naye akaruka na kutoka, akanikumbatia kiunoni, *hivi*, na kuniambia ya kwamba alikuwa ameachana na kazi yake hapo mjini, naye anaingia kwenye huduma ya umishenari, kama daktari mmishenari kwa watu. Na wakati alipokuwa akizungumza nami, alianza kunena kwa lugha zingine, alipokuwa akisema nami. Hiyo ni kweli, daktari wa tiba, Mwangilikana, Mwangilikana.

⁴⁵ Aliyefuata kule chini alikuwa ni mvulana mdogo, ama kijana mwanamume. Yeye... Sitakuwa na wakati wa kuingilia jambo hilo. Ni... Alikuwa ninii sana, i—ilimbidi kutembea kwa mikono na miguu yake, namna hiyo. Walikuwa wamemfunga mnyororo shingoni mwake, kama mbwa.

⁴⁶ Ndipo nikasema, “Jamani, wewe...” Maskini mtu yule, kama mtu yeyote angeweza kumsaidia, wala asingemsaidia, angekuwa ni mtu mwenye moyo mkatili sana. Nikasema, “Hakika, sasa, siwezi kumponya, mtu yeyote anajua jambo hilo. Siwezi kumponya. Ninaweza kusema tu kama Bwana atanionyesha kile kilichotukia, ama kilichousababisha, ama kitu fulani. Kwa maana uponyaji umenunuliwa tayari.”

⁴⁷ Sasa, ninawatakeni ninyi watu hapa, ambao ni wagonjwa, mtambue jambo hilo. Uponyaji umenunuliwa tayari. Mmeponywa tayari. Ni ukosefu tu wa imani. Mambo yote yanawezekana kwa hao watakaoamini. Inakupasa tu kuamini hilo sasa.

⁴⁸ Na kwa hiyo basi tunaona ya kwamba nanii huyu mdogo... jamaa huyu hapa, ni—nikasema, “Mleteni hapa juu.”

⁴⁹ Nao walikuwa wakimwongoza kwa mnyororo. Naye akawaza, sasa, wakati mwingine makabila hayo yanataka kuwafanyia watalii vichekesho. Nao wanacheza dansi kidogo, mwajua, dansi kidogo la kikabila, wapate sarafu kutoka kwa watalii. Naye akafikiri kwamba nilimtaka acheze dansi. Mvulana huyo hata hakuwa na akili timamu. Na, kweli, nisingeweza kusema kwenye umati huu uliochanganyana, maana hawavai nguo, mwajua. Wanawake wao, wanaume, na wote, wako uchi. Kwa hiyo wao—wao wanainii tu... labda ni tambara tu, ama chochote kile. Lakini alikuwa akitambaa

kwa mikono na miguu yake, na lilikuwa ni jambo baya sana. Kwa hiyo basi nili... Walimshika kwa mnyororo, namna *hiyo*, na wakamleta; walikuwa wameufunga shingoni mwake, mtu akimwongoza. Naye alikuwa akijaribu, akisema, “A-ba-ba-ba.” Nilijaribu kumfanya afahamu ya kwamba hicho sicho kitu nilichotaka. Mimi... .

⁵⁰ “Mkalimani wa Kizulu,” nikasema, “sasa sema maneno hayo. Mwambie asimame kimya na aamini tu.”

⁵¹ Ndipo akaniangalia namna *hiyo*. Na—nami nikasema, “Sasa, mvulana huyu ni... Amekuwa hivyo tangu alipokuwa mtoto mdogo sana.” Nikasema, “Kile ambacho kweli yeye ananinii... Kile anachowazia sasa, ni ndugu yake. Ndugu yake ama alikuwa amempanda mbwa wa manjano, ama mbuzi. Akarushwa mbali.” Kisha nikasema, “Akawa kiwete. Yeye hutembea na rungu mbili.” Halafu nikasema, “Sasa, ninaona ya kwamba mvulana huyo ameponywa. Yeye, ametupilia mbali mikongonjo yake.”

⁵² Panapo wakati huo, ilichukua dakika ishirini kuwanyamazisha. Mvulana huyo alikuwa ameketi umbali wa kama majengo matatu ya mji huko nje, huko chini upande *ule*. Huyu hapa anakuja, huku amebeba yale marungu kwa mikono yake, akitimua mbio tu kwelikweli kadiri alivyoweza. Alikuwa ameponywa, *huko* mbali kabisa, wakati yule mkalimani wa Kizulu. Wakalimani kumi na watano mbalimbali wamesimama pale. Unasema neno, inakulazimu kungojea mpaka lipitie kwa wakalimani hao. Huyu hapa anakuja, amebeba virungu hivyo kichwani mwake, namna *hiyo*. Alikuwa ameponywa.

⁵³ Na—na kisha ni—nikaangalia pande zote. Ndipo nikaona, tena, nikimwangalia, nikamwona akisimama. Hilo ni ono. Hakuna kitu kitakachokomesha hilo. La. Limekwisha tayari basi, unaona; linangojea tu neno.

⁵⁴ Sasa, angalieni. Jumatatu hii ijayo nitakuwa na umri wa miaka hamsini na mitano. Ni siku ya kuzaliwa kwangu. Nami nimeona maono tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Sijawahi kuona hata moja la hayo likishindwa. Nami nitamwuliza mtu yeyote kama wamepata kuona moja, lililoelezewa, likipata kushindwa. Haliwezi kushindwa. Ni Mungu.

⁵⁵ Kwa hiyo, ndipo nikalionga. Ndipo nikawazia, “Hii hapa nafasi yangu kupata ninii... ku—kufanya wito wangu wa madhabahuni. Nami nikamwona akisimama. Nilijua ataponywa basi, maana, mnaona, limekwisha kuonyeshwa tayari. Haina budi kuwa hivyo. Ni vile ono linavyosema. Hivyo ndivyo hasa lilivyo hasa.

⁵⁶ Ni wangapi wanajua ya kwamba mambo hayo ni kweli? Hili, wageni wapate kuona. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni kweli. Kamwe, haliwezi kushindwa. Mungu daima amelifanya kweli.

⁵⁷ Nikawaza, “Huu hapa wakati wangu wa kuita wito wa madhabahuni.” Nikasema, “Sasa, mvulana huyu hapa, siwezi kumponya. Lakini kama nguvu za Mungu zimenionyesha ono, basi ataponywa sasa. Sasa, endapo hataponywa, basi mimi ni nabii wa uongo. Lakini kama akiponywa, ni wangapi wenu huko nje mtampokea Kristo kama Mwokozi wenu binafsi?” Palikuwepo, nakisia, palikuwepo na Waislamu elfu kumi pale.

⁵⁸ Nilizungumza tu, siku chache kabla ya hapo, na mtu mwenye elimu. Kasema, “Hilo tuzo lililobarikiwa!” Unajua, wanatokana na Wamedi na Waajemi wa kale. Hawageuki wala kubadilika. Huwezi kumbadilisha mmoja wa jamaa hao.

⁵⁹ Kwa hiyo, nao hao hapo, wameketi pale. Mmoja wa wanawake hao wa Kiislamu alikuwa ndio kwanza amkubali Kristo, na hilo liliwashawishi. Na mwana wa Mahatma Gandhi alikuwapo hapo.

⁶⁰ Kwa hiyo, kulikuwa—kulikuwa na mvulana huyu. Na kwa hiyo nikasema, “Simama kwa miguu yako. Yesu Kristo anakuponya.” Vema, bado alijaribu kufanya, “Ug-ug-ug,” namna hiyo. Nilienda pale nikashika mnyororo huo kwa mkono wangu. Nikasema, “Simama. Yesu Kristo anakuponya.”

⁶¹ Sasa, hii hapa Biblia. Na kama nyote mnajua kilichotukia katika siku hizi chache usiku, nisingethubutu kusema jambo lolote ambalo lingekuwa ni makosa, katika jambo hili.

⁶² Hapo, huyo mvulana alikuwa ameteseka namna hiyo, alitembea, mgongo wake umebondeka ndani kabisa, kama farasi aliyebondeka mgongo. Mikono yake na miguu; mikono yake ilikuwa migumu kama miguu yake, kutokana na kutembea. Kwa mara ya kwanza maishani mwake, alisimama kwa miguu yake. Machozi yalitiririka kwenye tumbo lake jeusi, namna *hiyo*, yakatiririka tu, namna hiyo. Si kwamba tu aliponywa, bali akili zake zilikuwa timamu. Mnaona?

⁶³ Niliona, nikasema, “Sasa kwenu ninyi nyote ambao mtaamini, hebu na waamini sasa wakati nikiomba. Ninataka kujua ni wangapi hapa,” nikasema, “watamkubali Kristo kama Mwokozi?” Na ilionekana kama bahari. Nao wakaandikisha wenyeji elfu thelathini waliovaa blanketi, ambao hawakujua mkono wa kuume kutoka wa kushoto, waliomjia Kristo.

⁶⁴ Ninakumbuka nikiwahubiria Mabingwa wa Biashara, si muda mrefu uliopita. Halafu ninakumbuka jamaa aliyeiniweka wakfu hudumani katika kanisa la Kimishenari la Kibaptisti, ambaye daima alifanya mzaha. Nikasema, “Kile Wabapti-... Kile mnachoita ulokole, mnaona, kiliwaleta watu wengi zaidi kwa Kristo katika saa moja, kuliko makumi elfu ya dola ambazo kanisa la Kibaptisti limeweka katika wamishenari kule.

⁶⁵ Tuliwakuta na nini? Huko, wamebandikwa alama kama Mkristo, namna *hii*, huku wakibeba sanamu mkononi mwao. “Kama Amoya...” *Amoya* maana yake ni “nguvu

zisizoonekana,” kama vile upepo. “Kama akishindwa, *hii* haitashindwa.” Hiyo ndiyo nguvu yake. Na hapo niliona wenyeji elfu thelathini wanaovaa mablanketi wakiyatao maisha yao kwa Kristo.

⁶⁶ Na wakienda kwa makabila hayo huko nje, na kuwaongoa marafiki zao wengine kwa Kristo. Nami niliomba sala moja kwa kundi hilo lote. Na yapata muda wa karibu saa nne kutoka hapo, Sidney Smith, meya wa Durban, Sidney Smith, meya wa Durban, Afrika Kusini, alinipigia simu. Ambapo, kulikuwa na mwanamke aliyekuwa amekufa, usiku uliotangulia huo, nami nilikuwa nimeitwa, kuomba. Naye alikuwa mkutanoni, akiwa hai. Na kwa hiyo, basi, huyo alikuwa ni wa jamaa ya Sidney Smith, naye alikuwa amefurahi kwelikweli.

⁶⁷ Ndipo basi wakati hili, yeye alisema, “Nenda kwenye dirisha lako uangalie, kinachoshuka kuja barabarani.” Ndipo yakaja hayo malori makubwa, yamejaa tele. Nao wenyeji waliokuwa kwenye vitanda hivyo vidogo na machela, asubuhi hiyo, walikuwa wakitembea kwa nyuma, wameinua mikono yao, wakilia, wakiimba katika lugha yao ya kienyeji, “Amini tu. Mambo yote yanawezekana.” Wala hakuna vita tena miongoni mwao, ni safu tu baada ya safu ikishuka kuja kule. Malori yakienda namna hiyo, na magari ya polisi yaliyoyasindikiza, na ilibidi riksho zitimue mbio kila mahali, namna hiyo. *Amini Tu*.

⁶⁸ Sasa, kama wenyeji wanaovalia blanketi ambao hawajui mkono wa kulia wala wa kushoto anaweza kukubali jambo hilo, na sisi je? Mnaona? Mnajua ni kwa nini? Hawajapata kushindiliwa kasumba ya namna yoyote ya fundisho. Mnaona?

⁶⁹ Tumekuwa na kila mtu. Dk. *Fulani* anasema, “Ni ulokole.” Huyu mwingine anasema, “Ni telepathia.” Huyu anasema, “Hakuna lolote.” Huyu anasema, “Ni ibilisi.” Hujui la kuamini. Hiyo ndiyo sababu ni vigumu. Mahali pagumu kuliko popote pale pa kufanya ibada za uponyaji ni Marekani. Hiyo ni kweli.

⁷⁰ Kule, wao huko, hawajui kitu kuhusu hilo. Hawajasikia kitu. Nawaambia. Wao ni kama tu mtoto. Wanalikubali tu na kuliadini, nao hao wanaenda.

⁷¹ Bwana na atusaidie sasa. Sasa, na tuombe tu mara nyingine tena. Hatuwezi kuomba kupita kiasi, hilo ni jambo moja. Biblia ilisema, “Nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata.”

⁷² Tupokee, Bwana, katika ushirika Wako hapa, tunapojikabidhi Kwako, ushirika wa Neno Lako, kwa kuwa Wewe ndiwe Neno. Tunaomba katika Jina la Yesu, nenea mioyo. Amina.

⁷³ Tulimwacha Ibrahimu jana usiku katika... Tulianza naye, na hapa kwenye mlango wa 22 wa Mwanzo, ambapo alikuwa akimtoa sadaka mwanawe wa pekee, mfano wa Mungu akimtoa sadaka Mwanawe. Tulianza huko nyuma basi, tukarejea nyuma

kumchukua tena, maisha yake, nasi bado hatujaondoka kabisa kwenye jambo hilo. Tulimwacha, jana usiku, pale kwenye mlango wa 16 ama 17. Ninaamini, mlango wa 15 ndipo tulipomwachia. Nasi tutajaribu kulimalizia usiku wa leo, maana nina ujumbe kwa ajili tu ya uponyaji wa Kiungu, Bwana akipenda, kwa ajili ya kesho alasiri.

⁷⁴ Na sasa kila mchungaji anakaribishwa. Lileteni kusanyiko lenu. Njoni hapa mkasimame pamoja nao kwa maombi.

⁷⁵ Sasa tunatambua ya kwamba mara nyingine kwamba Yesu alifanya mambo, Naye hufanya mambo mara nyingine... Unasema, “Kwa nini aruhusu mambo haya basi, Ndugu Branham? Kwa nini aruhusu mambo haya kutukia?” Wakati mwingine yanafanywa kujaribu imani yako, mara nyingi. Sisi... Naye hufanya mambo yasiyo ya kawaida. Kwa nini Yeye asiondoke tu na kusema, “Mimi niko *Hivi*, Na niko *Vile*.” Yeye hakufanya hivyo mara ya kwanza. Unaona, anafanya jambo hilo kujaribu imani yako.

⁷⁶ Angalia, makuhani walifikiri ya kwamba labda Yeye angeshuka aje azungumze na Kayafa, kuhani mkuu. Lakini Yeye alizaliwa namna gani? Katika hori. Naye alikataliwa kabisa na watu Wake Mwenyewe na madhehebu Yake ya siku hizo.

⁷⁷ Sasa tunaona, wakati mmoja, Yesu akizungumza. Ningetaka tu kuangalia nukuu moja ndogo hapa ambayo ningetaka kuileta. Yesu amezungukwa na umati mkubwa, na ilionekana kana kwamba kulikuwa na wengi kupita kiasi, kwa hiyo angalia aliyosema. “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima.” Sasa unafikiri kwamba daktari wa tiba, ama msomi yeyote, wangepitia waliposikia Mtu ambaye alikuwa na jina la kuwa mwanaharamu na aliye zaidi sana kama kafiri kwa watu wa siku hizo, akisimama na kutoa nu—nukuu kama hiyo, “Msipoula mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu?”

⁷⁸ Mbona, wao wangesema, “Huyo Mtu ni kizuu kifyonza damu ya binadamu. Mbona, jamani! ‘Ati Kuinywa Damu ya Mtu, na kuula mwili Wake?’ Ninyi kusanyiko achaneni na Mtu kama huyo mwenda wazimu.”

⁷⁹ Yeye kamwe hakulielezea. Kamwe hakulielezea. Haikumbidi kulelezea. Hiyo ni kweli. Alitaka tu kuona walikuwa na imani ya aina gani.

⁸⁰ Mnaona, ninyi, kama mnaamini, aminini, sijali mtu yeyote anasema nini. Kama ningaliwaombea watu elfu tano usiku wa leo, na hao wote elfu tano wafe usiku wa leo, asubuhi ningekuwa bado nikiwaombea wagonjwa. Mnaona? Ni yale Mungu asemayo, ndiyo muhimu. Si kile watu wafanyacho. Mnaona?

⁸¹ Na, Mungu, Yeye—Yeye alisema, “Na msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.”

⁸² Vema, jamani, watu hao, kundi hilo la wasomi, mbona, mbona, wao walisema, “Achaneni na Mtu huyo. Ana kichaa. Amepotoka. Mbona, Yeye ni kizuu kifyonza damu ya binanadamu, ati ‘tule’ mwili wa Mtu huyo.” Sasa, Yeye kamwe hakulielezea.

⁸³ Sasa alikuwa na wahubiri sabini waliowekwa wakfu waliokuwa pamoja Naye. Alifikiri alikuwa kidogo na umati mkubwa wa watu kupita kiasi pale, kwa hiyo u—umati huo ukaondoka ukamwacha. Hivyo alikuwa na wahudumu waliowekwa wakfu wameketi pale, ambao aliwatuma, wahudumu sabini. Akasema, “Mtasemaje mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa Mbinguni alikotoka?” Sasa, Yeye kamwe hakulielezea hilo.

⁸⁴ Ndipo hao wahubiri wakasema, “Ati mtu huyu akipaa juu Mbinguni alikotoka? Mbona, sisi tunamjua. Tunajua mama Yake. Tumekuwako kwenye hori alimojaliwa. Tumeona susu alimobembemba. Tunavua samaki pamoja Naye. Tunakaa hapa ufukoni pamoja Naye. Na ati huyu Mwana wa Adamu ‘apae aende alikotoka?’ Yeye alitoka Bethlehemu. Liko wapi jambo hili la huku ‘kuja’? Hilo limetuzidi sana.” Ndipo wakaondoka wakamwacha. Kamwe hakulielezea. Hakulielezea kabisa.

⁸⁵ Haikumbidi kuelezea chochote. Haimlazimu Mungu kuelezea kitu chochote. Yeye ni Mungu. Yeye hulitenda tu, maana aliliahidi. Halifafanui.

⁸⁶ Ndipo wakabaki wale wa Kwake tu kumi na wawili. Ndipo akageuka na kuwaangalia, akasema, “Nimewachagua ninyi kumi na wawili, na mmoja wenu ni ibilisi.” Akasema, “Mnataka kwenda, pia?”

⁸⁷ Ndipo Petro akasema yale maneno makuu, “Tungekwenda kwa nani, Bwana? Kwa kuwa tuna hakika ya kwamba Wewe una Neno la Uzima.” Walikuwa wameliona limethibitishwa dhahiri kabisa; haidhuru makuhani walisema nini, yale mtu mwingine yeyote alisema. Walijua papo hapo, ya kwamba, ya kwamba Yeye alikuwa na Neno la Uzima. Alisema, “Wewe una Neno la Uzima.”

⁸⁸ Na sasa tunaona, haidhuru hao wengine walifanya nini, jinsi walivyoondoka, hao wanafunzi walikuwa wamechaguliwa tangu zamani, walikuwa wamekusudiwa Uzima wa Milele. La, wasingeweza kulielezea, wasingeweza kulielezea, si zaidi ya vile hao wengine walivyoweza. Lakini kulikuwa na kitu fulani ndani yao, ule—ule uwakilisho Mbinguni. Wazo ambalo Mungu alikuwa nalo juu yao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, lilikuwa limejidhihirisha lenyewe hapa, nao walikuwa wameunganishwa na Mungu na walikuwa na hakika ya kwamba hiyo ilikuwa ni ahadi ya Mungu iliyothibitishwa, wala hakuna kitu kitakachoibadilisha kutoka kwao. Huo ndio Ukristo halisi, wa kweli.

⁸⁹ Leo, watu wako katika hali kama walivyokuwa katika siku ambapo wanafunzi walikuwa huko baharini. Na usiku mmoja tufani ikaja, wala hakukuwa na kitu; matumaini yote yalikuwa yamekwisha, kwamba watapata kuokolewa. Nao wakamwona akija, akitembea juu ya ma—ma—maji. Sasa merikebu yao ilikuwa imejaa maji, na matanga yalikuwa yamevunjika, na makasia yalikuwa yameharibika, nao walikuwa wameshikana, wakipiga mayowe. Ndipo wakatazama huko nje wakamwona akija, akitembea juu ya maji, nao wakamwogopa. Tumaini lao pekee, nao walihofu kitu pekee ambacho kingeweza kuwaokoa. Kama hiyo si picha ya kweli leo hii, tena! Wao—walidhani ilionekana ni kitu kama pepo. Unajua, walisema walipaza sauti, kwa hofu, “Ni pepo!” Ilionekana sana kama ni kitu cha kiroho. Hivyo ndivyo ilivyo leo.

⁹⁰ Bali kama utafanya tu kama walivyofanya wakati walipopiga mayowe; walisikia sauti hiyo ikija, “Msiogope. Ni Mimi. Msiwe na hofu. Iweni na moyo wa ujasiri.”

⁹¹ Na kama utaangalia tu Neno la ahadi kwa ajili ya siku hii, utasikia sauti ile ile ikinena kupitia kwenye Neno, “Ni Mimi. Niliahidi kufanya jambo hili katika siku za mwisho. Msiogope. Msitishwe. Wekeni tumaini lenu Kwangu, Mwana wa Mungu,” kwamba Yeye ni Nani. Aminini hilo sasa.

⁹² Tulimwacha Ibrahimu Mbele za Elohimu, jana usiku, ambapo yeye . . . tulimleta kupitia kwenye ahadi mbalimbali. Na sasa ahadi ya mwisho kabla ya kule kuja kwa mwana, tunakuta kwamba Mtu mmoja alikuja; amevalia kama mwanadamu, akila kama mwanadamu, akazungumza kama mwanadamu; naye Ibrahimu akamwangalia na kumwita Elohimu, “Elohimu.” Wawili walikuwa wameshuka kwenda Sodoma, kuhubiri kule chini. Nasi tulifananiha hali hiyo na siku ya leo. Nyote mnakumbuka hadithi hiyo mahali tulipoiachia. Ni jambo lile lile kabisa kama vile Yesu alivyotabiri lingekuwa, ya kwamba, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” jambo lile lile liko mahali pale pale usiku wa leo. Na kama . . .

⁹³ Leo nilikuwa nimeketi pale, nami nilikuwa nikishangaa, nami nilishangaa sana kuhusu jambo hili. Walisikia tetemeko lingine la ardhi likitukia kule chini, nao wakasema, “Linatikisa nchi nyingi tena.” Nami nikawazia, ni kitu gani hiki? Mwajua, ilitendeka kwenye Ijumaa Kuu. Mwajua, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, kwenye Ijumaa Kuu, kanisa lilimkataa Yesu Kristo, na tetemeko la ardhi likaitikisa dunia nzima. Nao wamemkataa tena, katika Wakati wa Laodikia, kama vile Biblia ilivyosema wangepanya, walikuwa wamemtoa nje.

⁹⁴ Na mwenendo huu wa ekumeni wa Baraza la Makanisa ndivyo wanavyofanya hasa. Wanapoteza mafundisho yao yote ya kiinjilisti na kadhalika. “Watu wawili wanaweza je kutembea

pamoja wasipokuwa wamepatana?” Vema, huwezi kufanya hivyo.

⁹⁵ Hilo halitafanya kazi na Mkristo halisi, wa kweli. Hawatalipokea kamwe. La, bwana. Mkristo aliyezaliwa mara ya pili kamwe hataingia kwenye mtego kama huo. Ni kama tu kumweka bata ki—kizimbani. Wanajua anaelekea machinjioni. Kamwe hutaweza kumwingiza katika hicho. Kwa hiyo, sisi. . . Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili atakaa mbali na jambo hilo.

⁹⁶ Sasa Ibrahimu alikuwa amesimama pale naye alikuwa akizungumza na Mtu aliyekuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema alimokuwa Sara. Na ninii ya Abram. . . jina la Ibrahimu, siku moja ama mbili kabla ya hapo, lilikuwa ni Abram; na Sarai, na sasa ni Sara, kwa Ibrahimu. Naye alimwita Ibrahimu kwa jina lake la kibaba, la kikuhani. “Ibrahimu, yu wapi Sara (*binti mfalme*) mkeo?”

Akasema, “Yumo hemani, nyuma Yako.”

⁹⁷ Akasema, “Nitakurudia kulingana na ile ahadi, wakati huu huu mwakani,” kwa maneno mengine, “mwezi mwingine ujao. Nami nitakutembelea kama nilivyoahidi.”

⁹⁸ Amekuwa akimngojea mtoto huyu aliyeahidiwa kwa muda wa miaka ishirini na mitano sasa; bila kusita kwa kutokuamini Neno la Mungu, bali alipata nguvu, akimtukuza Mungu. Angalia jambo hili sasa.

⁹⁹ Na ndipo Sara, akiwa ndani ya hema, kama tungetumia msamiati wa mtaani, kwa namna fulani alicheka kifichifichi, kasema, “Mimi, mwanamke mkongwe, umri wa miaka tisini, na ati ni—nipate raha na bwana wangu, mume wangu, naye yuko huko mwenye umri wa miaka mia moja?” Walikoma kuwa kama mume na mke; miaka mingi, mingi sana.

¹⁰⁰ Na—na Mtu huyo, akiwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, alisema, “Kwa nini Sara alihoji hilo, akisema mambo haya moyoni mwake?” Unaona? Na kwa njia hiyo Ibrahimu alitambua ni Nani aliyekuwa akisema naye. Huyu alikuwa ni Elohimu, kabisa. Ishara Yake ilithibitisha dai Lake. Kasema, “Mimi nitakurudia.” Ni kwa nini alisema, “Mimi”? Alimwitaje Ibrahimu? Wakati, Yeye Ndiye aliyempa hilo jina. Katika mfano, si mbele ya mwanadamu; akionyesha yale yatakayotukia hasa. Kampa mamlaka yake iliyothibitishwa pamoja na Neno lililoahidiwa, ya kwamba Mtu huyu aliyekuwa akisema naye alikuwa ni Mungu, Elohimu.

¹⁰¹ Sasa tunaona, katika Waebrania mlango wa 4 na kifungu cha 12, kama nilivyolinukuu mara mbili, tayari, siku chache zilizopita usiku, ya kwamba, Biblia ilisema, “Neno la Mungu huyatambua mawazo yaliyo moyoni, siri za moyo.”

102 Na wakati Yesu angeweza kuangalia kusanyiko hilo na kuyatambua mawazo yao, na kumwambia mwanamke huyo ni waume wangapi aliokuwa nao, akamwambia Nathanaeli mahali alipokuwa, hilo lilikuwa ni thibitisho ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Masihi, Mungu, Imanueli, kwa kuwa alikuwa Neno.

103 Hivyo ndivyo manabii walivyokuwa. Manabii walihesabiwa kuwa ni miungu. Mnafahamu jambo hilo. Yesu alisema hivyo, Yeye Mwenyewe. Alisema, “Mnawezaje kunihukumu? Wakati, mnawaita hao waliojiliwa na Neno la Mungu, mnawaita ‘miungu’. Basi mnawezaje kunihukumu, ninaposema, ‘Mimi ni Mwana wa Mungu’? Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiamini hilo.”

104 Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililothibitishwa kwa ajili ya wakati huo. Sasa kama alikuwa amekuja na ishara ya Musa, isingalitenda kazi. Kama Musa angalikuja na ishara ya Nuhu, haikutabiriwa hivyo kwa ajili ya siku hiyo.

105 Na makasisi hawa wote, na theolojia, na shule za sekondari ya juu, na shule mbalimbali, na wahudumu walio na elimu; ambalo ni sawa, hatuna kitu dhidi yake, bali huo si Ujumbe wa saa hii. Huo ulikuwa ni kwa ajili ya siku ile ya utusitusi.

106 “Wakati wa jioni kutakuwako Nuru.” Yeye aliahidi mambo haya. Nimeyasoma na kuyasoma, kutoka kwenye Neno. Sawasawa kabisa na ilivyokuwa wakati huo, Yeye alisema itakuwa hivyo tena. Ningeweza kulihusisha na kila Andiko katika Biblia, na kuwaonyesha ya kwamba ni Kweli.

107 Sasa, madai Yake pale yalithibitishwa wakati aliposema kwamba nani, Sara, yale aliyofanya huko nyuma Yake. Sasa angalia, Yeye aliahidi, mwezi ujao atapata mimba, “wakati huu huu mwakani,” alisema.

108 Sasa angalia, njia ya Ibrahimu ilikuwa ni mfano wa Uzao wa kifalme sasa. Kama ukiangalia, Ibrahimu, ile ahadi ilikuwa kwake na kwa watoto wake baada yake. Halafu watoto wake walikuwa, kwanza, uzao wa maumbile ya kawaida, na halafu Uzao wa kifalme ambao ulikuwa ni Kristo. Uzao wa kwanza, ambao ulitokea kwa kujuana kijinsia, alikuja Isaka; bali bila ya jinsia, alikuja Yesu, Uzao wa Kifalme.

109 Sasa hiyo, ile Damu, unaona, tunaokolewa kwa Damu. “Na pasipo kumwagika damu, hakuna ondoleo.”

110 Angalia, Yesu hakuwa Myahudi. Yesu hakuwa Mmataifa. Yesu alikuwa ni Mungu. Hakuwa, asingeweza kuwa Myahudi wala Mmataifa. Angalia, jinsia ya mwanamume hutoa himoglobini, ambayo ni seli ya damu. Seli zazi iko kwenye seli ya damu.

111 Ninawasikia ninyi watu hapa, wengi wenu... Nilikuwa nikiendesha gari hivi majuzi, nikiwaangalia wakulima we—wenu, nanyi mna kuku. Sasa, kuku anaweza kutaga yai, maskini

mama ndege anaweza kutaga yai; bali endapo hajakutana na yule dume, halitaanguliwa kamwe. Hata hivyo, anaweza kutaga yai hilo, kwa kuwa yai hilo liko katika—katika . . . kwa yule wa kike. Lakini, ile damu, na uhai umo katika damu.

¹¹² Kwa hiyo, basi, uhai Wake ulikuwa ni uhai ulioubwa, si uliorutubishwa kutoka kwa mwanamume fulani.

¹¹³ Na halafu hilo yai halikuwa ni Mariamu, maana kama hilo yai lilikuwa ni Mariamu . . . Kama vile Waprotestanti wengi sana wanavyoamini, na Wakatoliki, pia, ya kwamba yai hilo lilikuwa ni Mariamu, sasa ninii . . . ati lilikuwa yai la Mariamu, likimfanya mwanadamu. La, kama seli hiyo ya damu ilikuwa ni Mungu, vivyo hivyo na yai pia lilikuwa ni Mungu, kwa maana Mariamu asingeweza kushusha yai hilo . . . Mwajua, mnafahamu yale ninayozungumzia. Yeye . . . Mariamu asingeweza kufanya jambo hilo bila ya mhemuko. Kwa hiyo, akiwa—akiwa na mhemuko, je! unamfanya Mungu anafanya nini basi? Itakuwa ni kujuana kimwili tena. Mnaona?

¹¹⁴ Kwa hiyo yai na seli ya damu pia ilikuwa ni Mungu. Amina. Hiyo ni . . . Amini jambo hilo, nawe utakuwa na imani ya kusonga mbele. Hatuokolewi kwa damu ya Kiyahudi, wala kwa damu ya Mataifa. Tunaokolewa kwa Damu ya Mungu, Mwenyewe, seli ya Damu iliyoumbwa.

¹¹⁵ Kama nilivyosema, wachukue hawa maskini mama ndege. Msimu wa kuchipua unakaribia. Nilikuwa nikiona hivi majuzi, jinsi ambavyo wanaokota majani makavu na kuruka juu na kutengeneza viota vyao. Sasa jike linaweza kwenda juu kule na kutengeneza kiota, na kutaga mayai kukijaza kiota hicho; na kuyaatamia, na kuyafunika, na kuwa mwaminifu sana kwa hayo mayai mpaka a—angedhoofika sana asingeweza kuruka kutoka kwenye kiota hicho, kujitafutia chakula. Lakini kama hajakutana na ndege dume, hayataanguliwa kamwe. Hayajarutubishwa. Mnajua hilo. Yatakaa kwenye kiota hicho, na kuoza.

¹¹⁶ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa baadhi ya makanisa yetu. Tuna kiota tu kilichojaa mayai yaliyooza. Hayana imani ya Ibrahimu. Ni wakati wa kusafisha kiota na kuanza tena, kukutana; si na madhehebu fulani, seminari fulani za kitheolojia. Bali ni kukutana na mume, Kristo Yesu, Ambaye huleta rutuba kwenye Roho wa Uzima aliye ndani yenu. Yeye ndiye anayekufanya uamini jambo Hilo. Safisha kiota na uanze tena. Mnawapapasapapasa mgongoni na kuwaingiza ndani, na kuwafanya mashemasi, na wameoa mara nne ama mara tano, na kila kitu. Ulimwengu unaelekea wapi, hata hivyo? Mnawapeleka seminari na kuwadunga baadhi ya hiyo giligili ya kuwafanya wasioze, na kuwarudisha.

¹¹⁷ Na hapa hivi majuzi, kwa kukisia, ilionyesha ya kwamba asilimia tisini na tisa ya wahubiri wa Kiprotestanti kote nchini,

hawaamini katika Kuja Mara ya Pili kwa Kristo katika mwili. Asilimia themanini na saba wanakana kuzaliwa na bikira. Wazia jambo hilo. Watoto wetu watakabaliana na kitu gani huko mbele?

¹¹⁸ Mungu, turudishe tena kwenye Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.

¹¹⁹ Ibrahimu, angalia njia yake anapokuja, alifananishwa na kanisa kabisa. Yote yale Ibrahimu aliyofanya, yameninii... Tumeliangalia kanisa. Kama tungalikuwa na juma moja ama mawili hapa, ya kuwa hapa, ningeweza kuwaonyesha, hatua kwa hatua. Kanisa limepitia njia ile ile. Ishara ya mwisho ilikuwa ni Mungu, Neno lililoahidiwa likisema naye, katika mwili wa kibinadamu. Ahadi ya mwisho kabla ulimwengu wa Mataifa kuangamizwa, ambao ulikuwa ni Sodoma na Gomora. Sasa wazieni, Ibrahimu, kabla, alikuwa...Mungu alikuwa amemtokea katika dalili nyingi, na nuru mbalimbali, na maumbile, na ishara, bali kamwe Mungu hakuwa amemjia kama mwanadamu na kuzungumza katika sauti inayosikika, kama mwanadamu, kutoka ndani ya mwanadamu. Na, kumbukeni, hiyo ahadi sasa iko karibu sana kutimizwa, Sodoma itachomwa moto, ujumbe wa mwisho unaendelea.

¹²⁰ Na ndilo hilo hapo kanisa la kawaida linasonga mbele, kanisa la kimaghehebu, hasa. Kule, kule anaenda Billy Graham wa kisasa kule, apate kuwavuta awatoe nje.

¹²¹ Hilo hapo Kanisa Teule, haliko Sodoma; lililoitwa litoke, likatengwa. Wanapata mjumbe. Angalia, kundi la Ibrahimu lilipata Ujumbe. Na sasa ilikuwa ni kitu gani? Mungu, aliyekuwa akiongea naye wakati wote, katika ishara na maumbile mbalimbali, na kila kitu, alikuja moja kwa moja. Na sasa anajidhihirisha papa hapa katika mwili wa kibinadamu, na anatambua wazo lililo katika moyo wa Sara, nyuma Yake. Naye Ibrahimu akasema, "Ni Elohimu, Yeye Anayejitosheleza kwa Yote." Kumbukeni, mara baada ya hayo, Sodoma ilichomwa moto. Wazia jambo hilo.

¹²² Huenda kanisa linapata ishara yake ya mwisho. Unaona, tumeninii... Mmepaza sauti, mmekuwa na kuhesabiwa haki kwa Luther; kutakaswa kwa Wesley, wakati mkuu, kupaza sauti, kushangilia; kunena kwa lugha, kufasiriwa kwa lugha, uponyaji wa Kiungu. Lakini tuko wapi sasa hivi? Mungu akinena moja kwa moja miongoni mwetu, kupitia kwetu, kwa sauti, kama tu alivyofanya kule. Naye aliahidi kufanya hivyo. Jambo ndilo hilo. Si kitu ambacho tulitunga. Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema angefanya jambo hilo, ajifanye Mwenyewe tena.

¹²³ Angalia, na mara baada ya jambo hili, Ibrahimu alimtetea Lutu. Naye alisema hata kama angepata watu kumi, asingeuangamiza. Lakini hata asingeweza kuwapata hao, hao wajumbe waliokuwa kule chini. Waliwakataa wale wajumbe.

¹²⁴ Ni kama kiamshakinywa cha Billy Graham, wakati alipokuwa kwenye mji wetu, huko Louisville, Kentucky. Nilikuwapo kwenye kiamshakinywa chake. Alisema, “Ninaingia kwenye jiji fulani,” akasema, “mimi...” Akainua Biblia. Yeye anaiamini sana Biblia. Akasema, “Ninaingia kwenye jiji na kufanya u—uamsho, ninapata waongofu elfu thelathini, ama wakata shauri.” Akasema, “Nami nitarudi, miezi sita baadaye, siwezi kukuta thelathini.” Kisha akasema, “Paulo aliingia kwenye mji na kumpata mwongofu mmoja, na wakati aliporudi, mwaka mmoja baadaye, huyo mwongofu alikuwa amewapata waongovu, waongofu mara waongofu, mpaka akawa na mamia ya waongofu kutokana na huyo mmoja.” Akasema, “Sasa kuna shida gani?” Akasema, “Ninyi kundi la wahubiri wavivu.” Akasema, “Mnaketi huku mmeweka miguu yenu juu ya dawati, wala hamtoki kwenda kuwatembelea watu hao.”

¹²⁵ Sasa mimi ni nani, mtu asiye na elimu kama mimi, kumpinga huyo mwinjilisti mkuu? Lakini ningalitaka kumwambia neno moja. “Billy, ni mhubiri gani aliyemchukua mwongofu wa Paulo.” Unaona?

¹²⁶ Ilikuwa ni kwa sababu Paulo alimzamisha kwenye kilindi vya kutosha, hata Kristo akaingia ndani yake naye alikuwa ni Moto ulio hai, moja kwa moja mpaka ndani kwenye Uwepo ulio hai. Si mhemuko fulani wa kiakili, ama mtu fulani wa kujiunga, ama kutia sahihi kumbukumbu fulani, ama mtu kuahidi atakuja kanisani. Mpeleke moja kwa moja kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, na ndipo yeye ata—atawaka Moto, atazaa watoto. Unawezaje kufanya hivyo mtu huyo akiwa hana mbegu za uzazi? Hawezi kuzaa watoto isipokuwa awe ana Uhai yeye mwenyewe. Na hiyo ndiyo njia pekee ambayo kitu chochote kinaweza kujizaa chenyewe, ni kwa njia ya seli zazi. Na hiyo seli zazi ni Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani ya Kristo, akiwa ndani ya mwaminio.

¹²⁷ Sasa tunaona, ishara ya Mungu ya mwisho kwa Ibrahimu, katika dhihirisho halisi, ilikuwa ni Mungu, Neno. Kumbukeni, Mungu lile Neno lililoahidiwa ambalo alikuwa ameahidiwa wakati wote, lilisema naye katika mwili wa kibinadamu. Mtu akiwa amesimama pale, akisema naye, akiyatambua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara; naye, akiwa yuko nyuma Yake, huko hemani. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho. Angalia sasa. Alikuwa amemtokea hapo siku zilizopita, katika ishara nyingi, na kadhalika, kama vile nuru mbalimali, na—na moto, na kadhalika, alimtokea, lakini sasa angalia. Na mara moja...

¹²⁸ Ninawatakeni mwone yale yaliyowapata hawa mume na mke wakongwe. Sasa natumaini hamnichukui kuwa ni mkereketwa fulani wa dini. Na—na endapo hamwamini hili, liacheni tu, hebu tu, unaona. Lakini ninataka tu kuwaambia yale ninayofikiria yalitukia.

129 Je! hivi mlipata kutambua sasa, jinsi Sara atakavyompata mtoto huyu mchanga? Sasa yeye ana umri wa miaka mia moja. Sasa mtu fulani anasema, “Vema, ilikuwa ni tofauti wakati huo.” Biblia ilisema ya kwamba tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa, na Biblia ilisema wote walikuwa ni wazee sana.

130 Lakini yeye anawafanyia Sara na Ibrahimu, tukija upande huu, kama tu vile alivvyoahidi kuufanyia Uzao wao. Naye amefanya hivyo! Ninaweza kuthibitishia jambo hilo, hatua zile zile hasa alizochukua Ibrahimu. Sasa hebu angalia mahali alipo hapa sasa wakati Mungu huyu alipokuja na kusema naye, katika mwili wa kibinadamu, akajitambulisha kwake. Mara moja sasa . . .

131 Sara atampataje mtoto huyu? Sasa Ibrahimu alikuwa ameishi naye, na labda alikuwa . . . Ilisema, “Mwili wake ulikuwa kana kwamba umekufa.” Biblia ilisema ulikuwa hivyo. “Mwili wake ulikuwa sasa umekufa. Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Lakini hakisita. Hata hivyo, yeye aliliamini.” Sasa angalia, kama Sara . . .

132 Niko katika kusanyiko lililochanganyikana, nanyi mnisamehe, akina dada. Nanyi mngemsikiliza daktari wenu; na mimi ni ndugu yenu. Lakini sasa angalieni. Sara, akiwa na umri wa miaka tisini, ni mkongwe sana asingeweza kuingia katika utungu wa kuzaa. Moyo huo usingeweza kuustahimili. Mnajua jambo hilo. Na jambo lingine, vena zake za maziwa zilikuwa zimekauka. Hawakuwa na chupa za afya na usafi katika siku hizo. Mnaona, ilimbidi awe ni mama wa kunyonyesha. Angalia. Kwa hiyo Yeye atafanyaje jambo hilo? Yeye atampataje mtoto huyu? Tumbo lake la uzazi limekufa. Mwili wake umekufa, yeye mwenyewe, na Ibrahimu amekufa.

133 Mnajua alilofanya? Yeye aliwabadilisha. Aliwabadilisha wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke. Naweza kuthibitisha hilo. Yeye aliwabadilisha wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke, akawageuza kuwa vijana tena. Loo, ni ahadi ya ajabu jinsi gani!

Mnasema, “Loo, Ndugu Branham!”

134 Vema, hebu ngojeni tu kidogo. Msininii . . . Tulieni tu. Hili linaweza kidogo likauma, kwa washika sheria, lakini na—nawatakeni mwone jambo hili sasa kwa muda kidogo tu. Sasa tunafundisha tu kama shule ya Jumapili juu ya jambo hili. Yeye aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke tena, wenye umri wa kama miaka ishirini.

135 Ibrahimu, sasa angalieni, yeye ni mzee. Masharubu yake yakining’inia chini kabisa. Mwili wake ni kama umekufa. Maskini mikono yake midogo, debwedebwe. Sara, maskini shali ndogo mgongoni mwake na kijikofia kidogo sana, maskini bibi kizee akienda kwa kuchechema kwa mkongojo.

¹³⁶ Ninaweza kuona kesho yake asubuhi. Mbona, Ibrahimu akiwa na nundu kubwa mgongoni mwake, mvi zikining'inia chini. Ndipo Sara akasema, "Ibrahimu, mpenzi, mbona, nde—ndevu zako zimegeuka zikawa nyeusi." "Mbona, Sara, hayo macho mazuri yanaangaza kama tu yalivyofanya siku zote. Mashavu yako yanapendeza sana." Kabla jua halijatua kesho yake usiku, alikuwa amebadilishwa kuwa kijana mwanamke tena, na yeye alikuwa kijana mwanamume.

Unasema, "Upuuzi huo, Ndugu Branham!"

¹³⁷ Loo, naam, ilikuwa hivyo, pia. Angalieni sasa ahadi ya ajabu na mfano kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, ikija mara moja. Kumbukeni, je! ni ahadi? Ndiyo, tutabadilishwa. Walibadilishwa wakawa kijana mwanamume na msichana, ikionyesha hasa jinsi Kanisa, Uzao wa kifalme, utakavyofanyiwa.

Mnasema, "Je! hiyo ni ahadi?"

¹³⁸ Wathesalonike wa Kwanza 4:17, "Parapanda ya Mungu italia, nasi tutabadilishwa mara tu, katika kufumba na kufumbua kwa jicho, tutanyakuliwa pamoja." Kwa nini? Mwili wake, miili yao, ilibidi ibadilishwe ipate kumpokea yule mwana. Na miili yetu inayopatikana na mauti, miili miovu itabidi ibadilishwe, ipate kumpokea Mwana, maana tutanyakuliwa. Itabidi tuwe na mwili tofauti na huu, kwa maana tutanyakuliwa hewani, kumlaki Yeye. Amina. Haipi-. . . Moja kwa moja tu na Maandiko, unaona. Walibadilishwa. Kama tutawahi kumlaki Bwana hewani, hatuwezi kumlaki tukiwa na mwili wa aina hii, maana sisi ni wa duniani. Lakini tutaupokea mmoja, haleluya, ambao utapaa juu katika Unyakuo.

¹³⁹ Na sehemu yake iliyo nzuri, ni kwamba jambo hilo liko karibu sana. Tunaona ishara zote zikiwa zimekaa sawa. Haitachukua muda mrefu sasa, moja ya asubuhi hizi kutakuwa na badiliko. Unaona?

¹⁴⁰ Lakini, kumbukeni, hilo litakuja tu kwa huo Uzao wa kifalme peke yake. Kuja kwa Yesu kutakuwa ni kwa siri sana, watu wengine hawatajua chochote juu yake. Je! hivi mnajua, labda hawatakuwa ni wengi mno. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." "Mlango ni mwembamba na njia imesonga, bali watakaoiona ni wachache." Unasema kutakuwa na mamilioni humo; naam, kote katika nyakati zote, waliokombolewa, hakika. Lakini, mahali hapo pa Kunyakuliwa, ambapo tunasimama sasa!

¹⁴¹ Ni kitu gani kitakachotukia moja ya siku hizi? Watasema, "Sasa, unajua, sisi hapa kwenye wakati wa ile Dhiki. Nilifikiri kwamba Kanisa lilikuwa linyakuliwe kabla ya wakati wa ile Dhiki." Hiyo ni Kweli. Si kanisa; Bibi-arusi. Kanisa linapitia kwenye wakati wa ile Dhiki, bali si Bibi-arusi. La, bwana. Yeye amekombolewa. Hana haja ya kutakaswa. Yeye ni safi

tayari. Roho Mtakatifu ameingia ndani Yake na kumtakasa, na kuondoa uchafu wote na takataka za ulimwengu, Naye analiamini hilo Neno na amekuwa sehemu Yake. Hiyo ni kweli. Bila ya Roho Mtakatifu, huwezi kufanya kitu. Ni Bibi-arusi anayetoka kwenye kanisa. Na pale, yeye, anayeitwa “masalia ya uzao wa mwanamke,” unaachwa upitie katika wakati wa ile Dhiki.

¹⁴² Unajua, wakati mmoja baada ya Maandiko yote, Isaya, Malaki 3, na Isaya 40, yakitabiri juu ya kuja kwa Yohana Mbatizaji. Yohana alikuja kulingana na hayo Maandiko kabisa. Na hata wanafunzi walimjia Yesu na kusema, “Kwa nini Waandishi hunena, Maandiko, ya kwamba huyo Eliya imempasa kuja kwanza?”

¹⁴³ Akasema, “Amekwisha kuja, nanyi hamkutambua hilo. Amekuja, nao wakamtenda tu yote aliyopaswa kutendewa, wala hamkutambua.”

¹⁴⁴ Sasa, hilo huenda likawa ni moja ya siku hizi, ungeweza kusema, “Na Unyakuo je?”

¹⁴⁵ “Umekwisha kupita, wala hamkutambua.” “Kutakuwa na watu wawili kitandani; mmoja atachukuliwa, mmoja ataachwa.” Unajua, kuna karibu watu mia kadhaa wanaotoweka duniani, kila siku, kwa vyovyote, mwajua. Watu hawajui ni kitu gani.

¹⁴⁶ Na wazieni tu jambo hilo, hiyo huzuni, kwamba watu wataendelea tu kuhubiri, na wakiadini wanaokoka.

¹⁴⁷ Na Nuhu aliingia kwenye safina, na mlango ukafungwa nyuma yake, kwa mkono wa Mungu. Jua likachomoza, kisha likatua, siku saba kabla ya jambo lolote kutukia. Nao watu waliendelea kuhubiri moja kwa moja, moja kwa moja wakidhihaki, na chochote kile, bila kujua ya kwamba rehema pekee waliyopata kuwa nayo ilifungiwa nje kwao.

¹⁴⁸ Wazia, wahudumu watakuwa wangali wakiwaelimisha wahubiri na kuwatuma kuhudumu, na mambo kama hayo yakiendelea, kanisa tu likisonga mbele; na pasipo na rehema kabisa, bila chochote, limekatiliwa mbali kabisa; Unyakuo umekwisha. “Mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu,” Maandiko yanasema hivyo. “Umekwisha kuja wala hamkutambua.” Wazieni juu ya jambo hilo, usiku wa leo, marafiki, na mwangalie yanayotendeka.

¹⁴⁹ Hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kukufariji sasa ila Neno la Mungu. Unaona? Hakuna matumaini mengine; taifa lenu, hakuna mahali pengine.

¹⁵⁰ Tumeliwa kabisa na mabuu. Mnajua hilo. Mabuu ya ukomunisti yamekula kitu hicho. Kinapaswa... Sharti liwe hivyo. Hamtalizuia. Biblia ilisema ilikuwa iwe hivyo, kwa hiyo hamtalizuia kamwe. Hivyo tu.

Iweni tayari kwa Unyakuo. Hilo ndilo jambo pekee la kufanya.

¹⁵¹ Wathesalonike, Wathesalonike wa—wa Kwanza 4:17 ilisema ya kwamba, “Tutabadilishwa,” kama Ibrahimu alivyobadilishwa, “na kunyakuliwa,” mwili wa tofauti. Sasa, Ibrahimu, miili yao mikongwe ilibidi ibadilishwe. Vivyo hivyo na yetu pia itabidi ibadilishwe, ili kuitimiza ile ahadi. Itabidi tubadilishwe. Sasa, unasema, ati miili hii mikongwe. Ninataka kuninii. . .

¹⁵² Nilikuwa nikizungumza kwenye Shirika fulani la Wafanyabiashara Mabingwa, hapa muda fulani uliopita. Na ninii—na daktari mmoja akatoka, baadaye, na kusema, “Bw. Branham,” kasema, “ninafurahia mazungumzo yako, ila,” kasema, “unajua, siwezi kuamini kwamba—kwamba—ya kwamba, kitu chochote, isipokuwa kiwe kinaweza kuthibitishwa kisayansi, kuhusu huko kuzaliwa na bikira na mambo kama hayo, na kuhusu kuwa Mungu.”

¹⁵³ Nikasema, “Vema, wewe kamwe hutamwamini Yeye, maana huwezi kumthibitisha Mungu kisayansi. Inakubidi kumwamini kwa imani, kwa imani.”

Akasema, “Vema, siamini kitu chochote kisicho cha kisayansi.”

Nikasema, “Je! wewe ni mwanamume uliyeoa?”

Akasema, “Naam, bwana.”

Nikasema, “Je! unampenda mke wako?”

Akasema, “Hakika ninampenda.”

¹⁵⁴ Nikasema, “Kisayansi nionyeshe upendo ni kitu gani basi. Ninataka kununua kiasi fulani, kama unaweza kuniambia ni duka gani la dawa linalouza. Kweli nina haja nao.” Nikasema, “Mimi. . .” Unaona, kitu rahisi tu.

¹⁵⁵ Nikasema, “Nitakuuliza swali. Sasa, hapa, je! tumeumbwa kwa mavumbi ya ardhi?”

Akasema, “Ndiyo, Bwana.”

¹⁵⁶ Nikasema, “Tunapokea mavumbi hayo kwa kula chakula kinachotoka ardhini, na ni uhai wa mimea, na kadhalika.”

¹⁵⁷ Unaona, unaweza kuishi tu kwa kitu kilichokufa. Unaona? Kama ukiishi, kitu fulani hakina budi kufa upate kuishi, kimwili. Kama ukila viazi ulaya, vilikufa. Kama ukila nyama ya ng’ombe, huyo ng’ombe alikufa. Kama ukila nyama ya nguruwe, nguruwe alikufa. Kama ukila mboga za majani, zilikufa. Ni namna fulani ya uhai. Nawe unaishi tu, kimaumbile, kwa—kwa nguvu za kitu kilichokufa. Kitu kilichokufa! Hivi kimantiki si ni dhahiri, rafiki, ya kwamba unaweza tu kuishi Milele kwa nguvu za kitu kilichokufa kwa ajili yako? Kristo alikufa, naam, akafufuka tena, kuthibitisha Uungu Wake. Angalia sasa.

158 Nikasema, “Daktari, kama nikila chakula basi, kila ninapokula chakula, kinaingia mwilini mwangu na kinatengeneza seli za damu.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

“Basi kila ninapokula, ninafanya upya uhai wangu.”

Akasema, “Hiyo ni kweli, seli mpya za damu.”

159 Nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani basi. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilikula mahindi na maharagwe na viazi na nyama, kama tu ninavyofanya sasa. Na kila wakati ninapokula, nilikuwa mkubwa zaidi na mwenye nguvu zaidi. Halafu basi nilipofikia umri wa kama miaka ishirini na miwili, kila mwanadamu, haidhuru unakula kiasi gani, jinsi unavyokula vizuri, unazeeka zaidi na kuwa mnyonge zaidi. Sasa kama ninamwaga maji kutoka kwenye kikombe *hiki*, kuyatia katika *hiki*, na nikijaze nusu; na halafu ninaendelea tu kumimina, baada ya kukijaza nusu; na badala ya kuongezeka, yanapungua. Nithibitishie kisayansi jinsi hilo linavyotukia. Unaona? Imekuwaje kwamba ninakula chakula kile kile, nikiyafanya upya maisha yangu kila siku, kulingana na... Inathibitisha, inathibitisha kisayansi ninafanya upya maisha yangu wakati ninapopata seli mpya za damu, damu ile ile niliyokuwa nayo nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita. Lakini ni kwa nini, baada ya mimi kufikia ishirini na kitu, basi haidhuru ninakula kiasi gani, ninashuka, ninakuwa mzee zaidi na zaidi na zaidi, na huku nikila moja kwa moja wakati wote? Badala ya kunijaza, kama kilivyofanya wakati huo, sasa kinanishusha chini.” Ni miadi. Hivyo ndivyo ilivyo.

160 Lakini Mungu alichora picha, naye alikupata wakati ulipokuwa kwenye umri wa kama miaka ishirini na kitu, kama hakuna kitu kilichoingilia kati kama maskini mvulana huyu kiwete anayeketi hapa. Ni kama tu shi—shina la mahindi lilivyoanza kukua, na kitu fulani kinalilalia na kulifanya likue kombokombo; kama unaweza kuondoa kitu hicho kilicholifanya kombo, shina hilo litanyoka. Halina budi kunyoka. Hivyo tu. Angalia, kama hakuna kitu kinacholiharibu, haya basi, msichana mzuri, mvulana mzuri. Wewe na mume wako mkisimama pamoja, Adamu na Hawa wa kisasa tangu mwanzo. Mungu alisema, “Hao hapo. Sasa ewe mauti wa—wafuatilie. Unaweza kuanza kuwachukua, bali huwezi kuwachukua kabisa mpaka nitakapoita.” Sasa ni kitu gani? Ni picha ya negetivu. Loo, jamani! Mnaona?

161 Hivyo hasa ndivyo alivyomfanyia Sara na Ibrahimu. Yeye aliondolea mbali uzee. Uzee ni ishara ya mauti. Wala hakutakuwa na ishara za mauti Mbinguni. Mnaona, kumbukumbu lote la mauti litaondolewa, wala hakutakuwa na uzee. Sote tutakuwa vijana. Ni picha tu ambayo Mungu ameichora katika ujana wako. Na sasa Mungu alimchukua

Ibrahimu na Sara na akawarudisha moja kwa moja kwenye huo umri mzuri wa ujana tena, kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo kwetu.

¹⁶² Pia thibitisho lingine ninalotaka kuwaonyesha sasa. Si—sininii...Ninahisi kwamba haliingii vizuri sana. Inanibidi kuninii tu...Hamwamini jambo hilo. Vema, hebu niwaulize. Hebu niwaonyeshe jambo fulani. Hebu niwaonyeshe ya kwamba kweli walifanya hivyo. Sasa angalieni.

¹⁶³ Angalia mahali walipokuwa, kwenye ramani, wakati Mungu alipowatokea, huko juu karibu na Sodoma. Mara baada ya hayo walifanya safari ya karibu maili mia tatu kwenda Gerari. Hiyo ni safari kwelikweli kwa mwanamume mzee na mwanamke. Huyu hapa mzee huyu sasa, huku masharubu yake yamening'inia chini kabisa, akitembea kwa fimbo yake. Huyu hapa maskini bibi kizee, mwajua, amevaa kijikofia, akiikokota miguu nyuma yake, akipiga hatua za inchi nne ama tano akitembea.

¹⁶⁴ Halafu basi, shida yake ilikuwa kwamba, wakati walipofika Gerari, kulikuwako na Abimeleki, mfalme mmoja aliyekuwa akitafuta mpenzi. Na hao wanawake wote warembo aliokuwa nao kule, wasichana wa Kifilisti; wakati alipomwona Sara, alimpenda, akataka kumfanya mke wake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ha-ha! Loo!

¹⁶⁵ Loo, ndugu, Biblia ni kama tu barua ya mapenzi. Inakubidi kusoma katikati ya mistari, uone inavyomaanisha. Mungu alisema, "Aliificha kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili, na akawafunulia watoto wachanga ambao wangejifunza."

¹⁶⁶ Wakati nikiwa huko nje hudumani, mke wangu huniandikia barua. Nami ninampenda, naye ananipenda. Naye anasema, "Mpenzi Bill, usiku wa leo hivi punde tu nimewalaza watoto kitandani. Nimefanya kazi leo." Ninaona kile yeye anachosoma, kile anachoandika. Lakini, unaona, ninampenda hivi kwamba, ninaweza kusoma moja kwa moja katikati ya mistari. Ninajua kile anachosema. Haimbidi kuniambia. Ninajua, maana ninaweza kusoma katikati ya mistari.

¹⁶⁷ Hivyo ndivyo ilivyo na Mungu, wakati usipojaribu kusoma kwa mtazamo wa kigazeti, msimamo fulani wa kitheolojia, bali upendane Naye. Shuka na kwa kweli umwingize moyoni mwako, "pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika moyo wao kwa Roho Mtakatifu," kisha anza kuisoma Biblia na utaiona ikitokea moja kwa moja katikati ya mistari. Unaona, unajua kile Yeye anachosema. Yeye hakusema hilo moja kwa moja katika Neno. Yesu alimshukuru Baba kwa maana alikuwa "ameyaficha mambo hayo kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili." Sasa, hakuna mtu mwingine angeweza kusoma barua za mke wangu namna hiyo, maana ninampenda hivyo, unaona, na hivyo ndivyo anavyoniandikia. Hivyo ndivyo Mungu anavyokuandikia. Ni katikati ya mistari, unalisoma.

168 Huyu hapa sasa, Sara, hakika, alishuka akaenda kule. Ungeweza kuwazia maskini bibi kizee, wajua? Na hao wasichana wote warembo kule katika—katika kundi la Kifilisti, katika nchi ya Gerari. Na huyu hapa Abimeleki pale, yeye ni mfalme kijana mwenye sura nzuri, naye anataka kujipatia mpenzi, kwa hiyo anatafuta kote kote. Wao ni warembo, na kila kitu. Lakini anamwona maskini bibi akija, unajua, akitetemeka, ana wasiwasi, akija, akasema, “Huyo ndiye nimemngojea. Huyo ndiye!” Kasema, “Loo!”

169 Ndipo Ibrahimu akasema, “Nakuomba, Sara, unionyeshe fadhili hii. Wewe unaonekana ni mzuri wa uso, unajua.” Kasema, “Utakapofika kule, useme mi—mimi ni ndugu yako, nami nitasema wewe ni dada yangu. Maana, usipofanya hivyo, wataniua na kukuchukua.”

170 Unaona, usingeweza kuwa na wake wawili kwa wakati mmoja wakati huo, unaona, kwa hiyo basi sisi. . . Asingeweza kuwa na waume wawili, hasa, wakati mmoja. Moja ya siku hizi, nitahubiri juu ya jambo hilo. Ndipo, nena kuhusu *Uzao wa Nyoka* ukichochea kitu fulani, ngojeni tu mpaka hili litakapotokea. Nini—nini, sasa? Kumbukeni.

171 Ndipo tunaona ya kwamba alipomwona huyo akija, maskini bibi huyo mzee namna hiyo, Abimeleki alimpenda, ndipo akaenda na kumchukua awe mke wake.

Wazia jambo hilo. Unaona mahali alipowarudisha? Hakika, ilimbidi afanye hivyo.

172 Biblia hii, barua ya mapenzi, ni kitu ambacho Mungu anatuandikia. “Ameificha kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili, Naye ataifunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza.” Yeye huficha. . .

173 Alificha kuja Kwake. Alimficha Yesu kwa Mafarisayo, hao wanafunzi wa Maandiko. Hatuna kitu cha kulinganisha nao leo. Haidhuru wao walikuwa wasomi jinsi gani, hawakumtambua. Alifichwa. Biblia ilisema alifichwa.

174 Na, mwajua, Biblia ilisema makasisi wa siku hizi wangefichwa vivyo hivyo. “Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiofanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, na wasiowapenda wale walio sawa. Wenye. . .”

Unasema, “Hao ni wakomunisti.” La, la.

175 “Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao.” Unaona? Hiyo ni kweli. “Hawa ndio wanaotoka nyumba kwa nyumba, na kuwaongoza wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa za aina nyingi,” na kadhalika. Angalia.

176 Sasa tunamwona Ibrahimu kule. Naye Abimeleki anamjia, akasema, “Huyo ndiye ambaye nimemngojea, wakati wote.”

Kwa hiyo aliwatuma wasichana wake waje kumchukua na kumpelekea huko, na, loo, labda wampambe vilivyo, na kumfanya aonekane kama malkia wa namna fulani. Na usiku huo...

¹⁷⁷ Ninawataka ninyi mwone hapa neema ya Mungu kwa nabii Wake. Hili linaweza likawasonga roho kidogo, bali ni Kweli. Haidhuru linaonekanaje, wewe angalia jambo hili ambalo Biblia ilisema.

¹⁷⁸ Sasa ninaweza kumwona Abimeleki, anafikiria, “Kesho nitamwoa msichana huyu mrembo wa Kiebrania. Naye yuko huko vyumbani kule sasa, na wapambe wangu wa malkia wanampodoa kwa manukato na kumtengeneza nywele zake vizuri, na kumpamba kwelikweli.” Sasa ungeweza kuwazia mwanamke mwenye umri wa miaka tisini akipambwa hivyo, apate kuolewa na mfalme kijana? Kwa hiyo tunaona kwamba, wakati wakimpamba msichana huyu mrembo wa Kiebrania vizuri sana, naye mwenyewe huku anaoga na—na kujilaza, na kunyosha miguu yake, baada ya kukariri sala zake, naye akalala, kasema, “Loo, jamani!”

¹⁷⁹ Sasa ungeweza kumwazia Ibrahimu akifanya ujanja wa namna hiyo, mwanamume ambaye angesema kitu kama hicho kuhusu mke wake? Nena kuhusu mwoga! Ibrahimu alifanya jambo hilo. Naye huko ameketi zake sasa, baada ya kufanya jambo kama hilo. Angalia.

¹⁸⁰ Ndipo Abimeleki, usiku huo Bwana alimtokea, katika ndoto, na kusema, “Wewe ni kama tu mfu.” Akasema, “Una mke wa mtu mwingine.”

¹⁸¹ Akasema, “Bwana, unajua ukamilifu wa moyo wangu.” Kasema, “Mimi—mimi... Yeye aliniambia huyo alikuwa ni ndugu ya—yake, naye akaniambia huyo alikuwa ni dada yake.”

¹⁸² Akasema, “Ninajua ukamilifu wa moyo wako, hiyo ndiyo sababu nikakuzuia usinitende dhambi. Unaona? Lakini huyo, mume wake, ni nabii Wangu.” Angalia neema Yake kwa nabii Wake, ingawa alikuwa makosani. Unaona? Kasema, “Yeye ni nabii Wangu. Sitayasikia maombi yako. Wewe nenda umrudishie mke wake; na umwache akuombe. Usipofanya hivyo, taifa lako lote limekwisha,” kila tumbo la uzazi lilifungwa. Wazia jambo hilo. Hivyo ndivyo alivyosema hasa. Naye Abimeleki alikuwa mtu mzuri, na alimcha Mungu. Naam, bwana.

¹⁸³ Lakini mnaona vile neema ya Mungu inavyofanya? Huyu hapo nabii Wake ameketi kule mahali fulani, ambaye alimtoa mke wake akaolewe na mtu mwingine, ingawa alikuwa akiitazamia ahadi ya mwana, na mambo kama hayo, nayo neema ya Mungu inadumu na Neno hilo haidhuru ni kitu gani. Hiyo ni kweli.

¹⁸⁴ “Mumewe ni nabii Wangu. Nami sitayasikia maombi yako. Hata uwe mwenye haki jinsi gani, na u mwadilifu jinsi gani, na

u mwerevu jinsi gani; asipokuombea, wewe ni mfu.” Kwa hiyo akamchukua na kumrudisha Sara. Loo, jamani!

¹⁸⁵ Ndipo Isaka akatokea kwenye jukwaa. Sasa katika kufunga, upesi sasa ninataka kuwapa jambo fulani. Isaka alikuja jukwaani na ndipo ile ahadi ikatimizwa.

¹⁸⁶ Sasa baada ya Isaka kuja, maskini mvulana huyo alikuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, na kadhalika, Mungu akamjaribu Ibrahimu maradufu. Alipokwisha kumjaribu, kwa muda wa miaka ishirini na mitano sasa, ndipo alimjaribu maradufu. Sasa akasema, “Ibrahimu, ninataka umchukue huyu mwana sasa, mwanao wa pekee, na umpeleke kwenye mlima nitakaokuonyesha hapa katika ono hili, nami ninataka umpandishe kule na umtoe sadaka.”

¹⁸⁷ Naye akasema yeye kamwe—kamwe hakukataa kufanya jambo hilo. Aliamka tu, kesho yake asubuhi baada ya Bwana kusema naye, akawatandika maskini wale nyumbu na kuchukua kuni na kadhalika, na kuzipasua, kisha akaondoka pamoja na wale nyumbu. Alisafiri siku tatu, na ndipo akafikia mahali pale, akaangalia kwa mbali, baada ya kufanya safari ya siku tatu. Sasa hapa ndipo Ibrahimu alipokuwa, na safari ya siku tatu. Na wakati mwanadamu wakati huo hakuwa na miguu ya petroli kama tulivyo nayo leo, na mtu yeyote wa kawaida anaweza kutembea maili ishirini na tano kwa siku. Mnaona? Alikwenda mpaka wapi, huko ndanindani kwenye hizo nyika?

¹⁸⁸ Naye akasema, “Sasa ninyi ngojeni hapa.” Ninapenda jambo hili kumhusu Ibrahimu. Aliwaambia hao watumishi, akasema, “Ngojeni hapa pamoja na hawa nyumbu, na mimi pamoja na mwanangu tutaenda huko ng’ambo tukaabudu, nasi tutarudi.”

¹⁸⁹ Atafanyaje jambo hilo, wakati alipanda kule juu apate kumwua? Mungu alimwambia, akasema, “Panda huko juu na ukautoe uhai wake.”

¹⁹⁰ Lakini Biblia ilisema nini, katika Warumi 4? “Ibrahimu alijua ya kwamba alikuwa amempokea kama mfu, na alihasabu kabisa ya kwamba Mungu anaweza kumfufua hata kutoka kuzimu, kutoka kule alikompata kama mfano.” Unaona?

Akasema, “Ninyi ngojeni hapa.”

¹⁹¹ Itakuwaje, siwezi kuwaambia. Unaweza kuwazia jambo hilo wewe dada uliye na mtoto mchanga mikononi mwako, na mama unayeketi kwenye kiti cha magurudumu, mvulana mdogo pale, huku baba fulani? Sijui jinsi atakavyofanya jambo hilo. Sijui tu ni vipi atakavyolifanya. Lakini atalifanya kwa sababu Yeye aliahidi angelifanya, kwa msingi kwamba wewe ungeamini. Yeye huwafanyia wengine. Mnaona?

¹⁹² “Mimi na mvulana huyu, mimi na kijana huyu, tutawarudia. Unaona, ninyi ngojeni hapa, nasi tutaenda kuabudu.”

¹⁹³ Ndipo akambebehesha maskini Isaka hizo kuni, mfano wa Kristo akibeba msalaba Wake. Wakafika juu ya mlima. Ndipo maskini Isaka akaanza kushuku, naye akasema, “Babangu?”

Akasema, “Mimi hapa, mwanangu.”

¹⁹⁴ Akasema, “Mbona, madhabahu yapo, moto upo, kuni zipo, bali yuko wapi mwana-kondoo wa sadaka?”

¹⁹⁵ Sikilizeni maneno haya sasa yakitoka katika kinywa cha Ibrahimu. “Mwanangu, Mungu atajipatia Mwenyewe mwana-kondoo kwa hiyo sadaka.” Hilo linamaanisha, “Sadaka iliyotolewa na Mungu,” *Yehova-Yire*. Mwana-kondoo aliyetolewa na Bwana.

¹⁹⁶ Na wakati alipoifunga mikono yake na kumweka juu ya ma—madhabahu, wazia sasa huo ulikuwa ni wakati wa jinsi gani. Baada ya kumngojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano, ndipo Mungu akamfanya, akamwagiza kuangamiza kitu pekee alichokuwa ameshuhudia habari zake miaka hiyo yote. Alikuwa ni fedheha miongoni mwa watu, wakimcheka. Na hapa Mungu anasema, “Angamiza kitu kile chenyewe ambacho kitakupa tumaini la pekee uwezalo kuwa nalo, ya kwamba Neno Langu litatimizwa ndani yako. Ninakupa mvulana huyo. Yeye ana umri wa miaka kumi na miwili. Wote wamemtambua, lingali lilikufanya baba wa mataifa, bali nenda ukamwue mvulana wako.” Ungeweza kuwazia jambo hilo?

¹⁹⁷ Mungu akituonyesha tu. Haidhuru mtu yeyote anasema nini, ama jambo lolote kinyume cha Neno hilo, usikubali kuliangalia. Uzao halisi wa Ibrahimu unaamini jambo Hilo.

“Mwangamize huyo mwana.”

¹⁹⁸ Ndipo Ibrahimu akamlaza pale juu. Unaweza kuwazia, akishika maskini nywele zake za kipilipili na kuzifingirisha zitoke usoni mwake. Na macho yake madogo ya hudhurungi yakiangalia juu namna *hiyo*, na midomo yake midogo ikitetemeka. Anaona kisu hicho kikubwa chenye ubapa kikitoka kwenye ninii ya baba yake...Hebu wazia juu ya baba. Alisukuma kichwa chake nyuma, na kuvuta shingo yake nyuma ili aweze kumkata koo kwa kisu hiki. Loo, katika utii wa Mungu! Haidhuru ilionekanaje, yeye alisema, “Nilimpokea kama mtu aliyetoka kwa wafu. Mungu anaweza kumfufua.” Akainua kisu nyuma na akaanza.

¹⁹⁹ Ndipo Roho Mtakatifu akaushika mkono wake, kasema, “Ibrahimu, Ibrahimu!”

Akasema, “Mimi hapa.”

²⁰⁰ Akasema, “Usiunyoche mkono wako.” Kasema, “Ninajua ya kwamba unanipenda na unaniamini sasa, kwa kuwa hata usingeninii... Ungenipa mwanao wa pekee.”

²⁰¹ Na yapata tu wakati huo, kulikuwa na kondoo dume amenaswa pembe zake, nyikani, nyuma yake.

202 Ninataka kukuuliza jambo fulani, ndugu, dada. Huyu kondoo dume alitoka wapi? Angalia, mtu uko kule nyuma, safari ya siku tatu mbali na watu, huko nyikani, ambako kuna simba, mbwa mwitu, na kila namna ya mbwa mwitu na hayawani, na vitu huko nyikani vingemwua huyo kondoo dume mara moja. Pia, angalia, yeye yuko huko juu kabisa mlimani ambako hakuna maji. Naye alikuwa ameokota mawe kote katika eneo lile, akijenga madhabahu hii, wala huyo kondoo dume hakuwako. Lakini wakati Mungu alipohitaji mmoja, huyo hapo. Wala halikuwa ni ono. Alimchoma kisu na damu ikatiririka kutoka kwake. Akafa. Mungu alimnena akawa hai dakika hii, naye Ibrahimu akamtoa uhai dakika iliyofuata. Unaona? *Yehova-Yire*, “Bwana atajipatia mwana-kondoo.”

203 Jambo lisilowezekana kwa kondoo dume kuwapo pale. Kama mtu yeyote anajua kuhusu kondoo msituni, katika nyika kama hiyo, ndani kule ambako wanyama mwitu wote na vitu vikatili huko nyuma vingemwua huyo kondoo dume sasa hivi. Asingeweza kuishi huko ndanindani. Na hapa, juu ya kilele cha mlima ambako hakuna maji, hakuna nyasi wala chochote juu kule, wala hakuwako kule dakika chache kabla ya hapo. Na katika wakati tu ambapo Mungu alimhitaji kondoo huyo dume, huyo hapo; Yeye alimnena akawa.

204 Ni kama tu vile alivyomtokea kule. Elohimu, Yeye alihitaji mwili, alihitaji mwili wa kushuka kuja duniani nao, kwa hiyo alikusanya tu nurulimwengu na petroli, na kadhalika, kisha akaingia ndani yake. Unaona, Yeye ni Mungu.

205 Hivyo ndivyo atakavyokufanyia wewe, baada ya wewe kuwa si zaidi ya kijiko kimoja cha majivu mavumbini. Yeye bado atanena, nawe utatokea. Ataliita jina lako, nawe utaitika. Uzao wa Ibrahimu, ni ninii ya jinsi gani . . . ahadi hiyo kutimizwa.

206 Angalia, ilikuwa ni kondoo dume. Sasa kama mna dakika moja tu zaidi, ningetaka kuelezea jambo hili. Mnajua, hivi juzi usiku sikuligusia. Hata sijapata kulielezea kwa kanisa langu. Kumbukeni wakati alipothibitisha dhabihu hiyo, alipomthibitishia agano hilo; akichukua mbuzi jike, akachukua ndama (ng’ombe jike mdogo), na kuwapasua vipande viwili, kisha akamchukua kondoo dume. Sasa, kumbukeni, wakati Uzao wa kifalme wa imani Yake, kumbukeni, haikuwa ni wa kike, ilikuwa ni wa Kiume. Ilikuwa ni wa Kiume, ile ahadi imetimizwa. Angalia, kondoo dume, dume; Mume, kuendana na Neno. Yeye ni Neno, yule Kondoo Mume, si wa kike. Walitolewa dhabihu kwanza, kumbukeni, Mwanzo 15, hao wa kike; walikuwa wa kwanza kuchinjwa; kisha akamchukua kondoo dume. Kondoo mume alikuwa ndiye wa mwisho. Yeye, Kondoo Mume, Neno lililotolewa; si mbuzi jike, dhehebu, kanisa. Mnaona? Si wa kike, kanisa; bali Mume, Kondoo Mume. Amina. Hiyoni ndiyo sababu alizaliwa Aprili.

207 Sio Desemba kama vile kanisa la Kirumi linavyoliweka, siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua, na kuiweka pamoja na Yake, kule juu kwenye tarehe ishirini na tano Desemba, wakati sarakasi zao zilipokuwa zikiendelea, kama umewahi kuchukua ni—ninii... mmesoma historia ya kanisa. Nanyi mnafahamu ya kwamba waliweka hiyo huko juu, kuifanya... Ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa mungu jua, jua, wakati linasimama karibu kimya. Halibadiliki kwa siku tano, kutoka Desemba ishirini mpaka ishirini na tano. Waliweka siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu na ya mungu-jua pamoja, wakiupatanisha Ukristo na upagani, wakaifanya Desemba. Asingeweza kuzaliwa Desemba ishirini na tano, kwa nini, milima imejaa theluji huko juu Uyahudi.

208 Yeye alizaliwa kama ilivyo wana-kondoo wote. Alizaliwa katika msimu wa kuchipuka majani. Na ilibidi azaliwe chini ya kondoo dume, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Kondoo Mume, na kondoo dume ilikuwa ni Aprili. Kweli kabisa. Alizaliwa chini ya huyo kondoo dume. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Yeye alikuwa ni Kondoo Mume wa Mungu. Alikuwa Ndiye huyo kule mlimani aliyepachukua mahali pa Isaka. Amina. Hivi hamwoni jambo hilo?

209 Hilo hapo, inaonyesha hapa dhahiri, Bibi-arusi Uzao wa kifalme hataitwa kwa wa kike, kanisa, dhabihu ya mbuzi jike wa kimadhehebu. La. Bali kwa Yeye, Neno lililodhihirishwa la Kondoo Mume, Kwa maana Yeye ni Neno na Kondoo Mume, basi. Si kuitwa, Yeye alisema, si kuitwa kwa jina *lake mke*, bali, "Kuitwa kwa Jina *Lake Mume*. Yeye angechukua watu toka kwa Mataifa," si kwa jina la mke, bali, "kwa ajili ya Jina Lake Mume," wangeitwa kwa Jina Lake. Loo, jamani! Kwa nini unaliogopa jambo hilo, basi? Mmataifa angeitwa kwa Jina Lake, Kondoo Mume; si jina lake mke, kanisa. Si mwanamke; bali Mwanamume! Haleluya!

210 Uzao wa kifalme ungeliona Hilo. Hivi huwezi kuona Malaki 4 ikija kutimia? "Kurudisha Imani ya asili, Neno la Mungu!" Hakika ninyi watu mnaweza kuona jambo hilo. Haitatubidi kulifanya dhahiri zaidi. Achilia dhehebu hilo. Ewe mtu, rudi kwenye Neno hilo. Na Sauti ya siku ya mwisho, na ishara ya siku ya mwisho, ni ya kuwarudisha watu kwenye Imani ya asili, Malaki 4 ilisema hivyo, kurudi kwenye Neno.

211 Naye alikuwa Neno, si mwanamke; Mwanamume, amina, Jina la Bwana Yesu; Neno lililothibitishwa sasa kwa ahadi, Neno lililoahidiwa.

212 Yohana Mtakatifu 14:12, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Malaki 4, ilisema jambo lile lile pale. Pia, Luka 17 inatwambia, ya kwamba, katika siku za mwisho dhihirisho la ulimwengu litawekwa katika utaratibu kabisa, "kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," naye Mungu

angeshuka, akidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, naye angejua siri za mioyo. Hmm, hmm. Yesu alisema jambo hilo, na lingetukia, “katika siku ambazo Mwana wa Adamu anafunuliwa,” mwishoni mwa ulimwengu.

Unaona, si kanisa, “Jiunge na *hili*, jiunge na *lile*.”

213 Hilo ni kusema, njoni Kwake! Hilo ndilo uzao wa Ibrahimu ulilopata kule, dhabihu iliyotolewa, badala ya uzao wake wa maumbile ya kawaida. Na Uzao wake wa kiroho je, amina, Uzao Wake wa kifalme, Uzao wa Malkia? Amina. Loo, Laiti tu mngaliweza kuliona hilo! Kumbukeni, ni kitu gani? Ni mwili na Roho vikiungana, vikifanyika mmoja.

214 Angalia katika Mathayo, mlango wa 3. Huu hapa mwili, Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira, akishuka kutoka m—mjini, akamwendea Yohana Mbatizaji.

215 Basi alikuwa ndiye huyo hapo, akisimama majini. Biblia ilisema, “Neno la Bwana daima humjia nabii.” Hiyo ni kweli? Naye Yohana alikuwa ni nabii. Hawakuwa wamepata nabii katika mamia ya miaka.

216 Lakini alikuwa ndiye huyu hapa, nabii amesimama pale, naye alikuwa akitabiri ya kwamba Yesu angekuja. Alikuwa huko jangwani, naye akasema aliona ishara. Mungu alimwambia ya kwamba ishara hiyo ingekuwa ikimfuata huyo Masihi, atakapokuja. Yeye alisema, “Amesimama miongoni mweni mahali fulani sasa. Yupo Mtu miongoni mwenu, ambaye sistahili kufungua viatu Vyake. Atadhihirishwa moja ya siku hizi. Na atakapodhihirishwa, basi mimi nitapungua, Yeye ataongezeka.”

217 Ilitokea kwamba aliangalia, ndipo akaona ishara hiyo; akasema, “Huyu hapa anakuja sasa. Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.”

218 Yule mhubiri mzee wa Kibaptisti, Daktari Davis, aliyenibatiza nikaingia katika ushirika wa kanisa la Kibaptisti, alilizungumza jambo hilo pamoja nami wakati mmoja. Akasema, “Unajua kilichotukia pale, Billy?”

Nami nikasema, “La, sijui, Daktari.”

219 Akasema, “Hivi ndivyo ilivyotukia. Yohana hakuwa amebatizwa kamwe.” Kasema, “Yohana alimbatiza Yesu, kisha Yesu akageuka na kuambatiza Yohana.”

Nikasema, “Si—sijui juu ya jambo hilo.”

220 Kwa hiyo nilidumu kuomba kuhusu jambo hilo. Usiku mmoja katika ono, hivi ndivyo ilivyokuwa. Unaona? Yeye kamwe, kamwe, Yesu kamwe hakumbatiza Yohana. Vema, nini?

221 Alisema, “Mimi ninahitaji kubatizwa na Wewe, basi kwa nini unakuja kwangu?”

Yesu akasema, “Kubali kwamba iwe hivyo.”

222 Angalia macho hayo mawili, watu wawili muhimu duniani; *huyo* hapo Mungu, *huyo* hapo nabii Wake, na Neno likamjia nabii. Kama Neno liko katika mwili, litamwendea nabii. Haidhuru liko wapi, litamwendea nabii. Halina budi kufanya hivyo. Biblia ilisema hivyo. La... na hili hapa linakuja... Yeye alikuwa Neno. “Hapo Mwanzo kulikuwako Neno. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Na hili hapa Neno linamjia nabii, moja kwa moja huko majini, kutimiza na kuthibitisha unabii wake. Amina. Huyu hapa amesimama pale, na hapa hayo macho mawili yakikutana; mmoja ni nabii, na huyo mwingine ni Neno.

223 Naye, Yohana, akijinyenyekeza mbele Zake, alisema, “Nina haja ya kubatizwa na Wewe, basi kwa nini Wewe waja kwangu?”

224 Akasema, “Kubali iwe hivyo, kwa kuwa ndivyo itupasavyo,” tunapaswa, unaona, “itupasavyo kutimiza haki yote.”

225 Yohana, akiwa nabii na alijua hilo Neno, maana Neno lilimjia yeye, alijua ya kwamba huyo alikuwa ndiye ile Dhabihu. Na kulingana na Torati, Dhabihu ilipaswa kuoshwa kabla haijatolewa. Ni kweli kabisa. Yeye alimbatiza Yesu kwa sababu Yeye alikuwa ndiye dhabihu ijayo. Kabla hajaingia kwenye maisha Yake ya umma, ilibidi abatizwe, kwa sababu dhabihu haina budi kuoshwa kabla haijatolewa. Amina. Naye akambatiza.

226 Na alipofanya hivyo, alitoka mara hiyo majini. Ndipo akaangalia juu na kumwona Roho wa Mungu, kama hua, na sauti ikitoka Kwake, ikasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ninayependezwa kukaa ndani Yake.” Mungu na mwanadamu wakawa mmoja.

227 Adamu na Hawa walikuwa mmoja, hapo mwanzo. Na wakati alipowatenganisha, mwanamke alianguka, kwa sababu ya Neno. Alilikosa Neno. Akaanguka.

228 Vivyo hivyo na kila wakati wa kanisa, unaanguka namna hiyo, kwa sababu ya kufasiriwa vibaya kwa Neno. Kumwacha yule mfasiri, yule Shetani aliyemfasiria Hawa, “Loo, hakika *Hilo* lisingeweza kuwa kweli. Hakika *Hili*, hakika yote *haya* hayawezekani. *Hili* haliwezekani. Loo, naam, ninajua, hakika...”

229 Lakini kama Mungu alisema hivyo, hilo hulifanya kweli. Hakuna cha kusema “hakika” yoyote Kwake. Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kumpokea Roho Mtakatifu. Ni hivyo, la sivyo utaangamia! Angalia.

230 Na hapa Yeye—huyu hapa anaingia, Yesu na Mungu wakawa mmoja. Waliungana.

231 Kama vile kule Edeni, ambako kule Adamu na Hawa walikuwa hapo mwanzo, roho mmoja. Waliitwa majina yao Adamu. Unaona? Yeye alikuwa wote wawili Adamu na Hawa,

pamoja. Na walipotenganishwa, wapate kuingia majaribuni, nini kilitukia? Hawa alianguka, kwa Neno. Hilo lilikuwa Neno. Adamu alienda kumtafuta, apate kumkomboa, bali asingeweza kumkomboa. Hakuwa anastahili kumkomboa.

²³² Ndipo akaja Adamu wa Pili, kulikomboa Kanisa, ambalo lilikuwa ni katika kivuli na mfano.

²³³ Sasa, hakika tu kama vile ilivyowabidi Adamu na Hawa kuwa roho yule yule, Kristo na Kanisa hawana budi kuwa ni Roho yule yule, huduma ile ile. “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Mnaona ninalomaanisha? Ilibidi waungane pamoja. Mwili na damu, na Mungu, ilibidi waje pamoja na wawe Roho mmoja. Naye Yesu Kristo na Kanisa Lake ni Roho mmoja. Kanisa linawezaje kukana uumbaji, kanisa linawezaje kukana jambo ambalo Kristo aliwaambia wafanye, tunawezaje kukana jambo Hilo na halafu tuseme kwamba sisi ni wa Kristo? “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtapewa. Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi, na Uhai ulio ndani ya mzabibu huingia ndani ya tawi lipate kuzaa tunda.” Wazaa matunda!

²³⁴ “Na kila tawi lisilozaa tunda zuri, hukatwa.” Hivyo ndivyo madhehebu yalivyofanya, yalilivunja-vunja, yakalichanganya Neno, na kuanza namna hiyo. Na mmoja anaanzisha moja *hivi*, na mwingine *vile*, na, muda si muda mwajua, kundi dogo la akina riki linaingia na kutia wazo lao ndani yake, na, muda si muda unajua, ndipo linakuwa ni kundi kubwa tu la Babeli. Yeye analikata tu.

²³⁵ Hakuna madhehebu yaliyopata kuinuka, pasipo kuanguka. Na kila moja lililoanguka, kamwe halikuinuka tena. Ninampa mtu yeyote changamoto hiyo. Naam, bwana. Mnajua historia. Hapajakuwa na moja kamwe. Mungu, mara wanapounda madhehebu, Yeye anayaweka kwenye rafu, na huo ndio mwisho wao. Atamchukua mtu kutoka mahali pengine, alitoe nje moja kwa moja. Hakika.

²³⁶ Angalia katika hili sasa, inawabidi kuwa mmoja. Yesu alisema, basi, “Uhai ulio ndani Yake utakuwa katika Kanisa Lake.” Na hili hapa lile hasa aliloahidi katika siku za mwisho, ya kwamba Uhai uliokuwa katika Kristo, uliokuwa katika... utadhihirishwa katika siku ambazo ulimwengu uko katika hali ya Sodoma kama tu ulivyo sasa. Hivi huwezi kuona, ndugu, dada?

²³⁷ Inafaa nini kujiunga na kanisa kama huna Kristo maishani mwako, na Kristo akijitambulisha Mwenyewe maishani mwako? Unaona, ndilo jambo lenyewe hasa. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yeye alisema hivyo. Ungewezaje kusema hivyo, kama sivyo, unawezaje kudai kwamba wewe ni wa Kristo?

238 Unasema, “Ndugu Branham, unafikiri utawezaje kulifanya hilo litie nanga ndani ya watu, katika siku hii ya kielimu wakati kila kitu ni madhehebu?”

239 Nilimwuliza mwanamke mmoja, si muda mrefu uliopita, “Je! wewe ni Mkristo?” Hospitalini. Akasema, “Nataka ufahamu ninawasha mshumaa kila usiku.” Kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote na Ukristo? Nilikuwa . . .

240 Nilienda kumwombea mwanamke mwingine, nami . . . mama mwingine alikuwa amelala pale, akiwa mgonjwa, yeye na mwanawe. Nami nikasema . . . Niliingia. Nikasema, “Mama, hivi wewe . . . Naam,” nikasema, “Ninakujua wewe ni nani. Wewe ni Bibi Oliver.”

241 Akasema, “Naam, Ndugu Branham.” Akasema, “Nimekuwa mgonjwa sana, Ndugu Branham. Daktari hawezi kuona shida yangu ni nini. Naomba unifanyie maombi? Hiyo ndiyo sababu nilikupigia simu.”

242 Nikasema, “Hakika, Dada Oliver.” Nikasema, “Unaweza kuinamisha kichwa chako?”

243 Kasema, “Hebu kidogo! Funga hilo pazia!”

244 Ndipo nikasema, “Vema, sawa.” Nikasema, “Nilitaka tu kuomba. Je! *wewe* ni Mkristo?”

Akasema, “Sisi ni Methodisti.”

245 “Vema,” nikasema, “hilo silo nililokuuliza. Nilikuuliza kama ulikuwa Mkristo.”

Akasema, “Funga hilo pazia!”

246 Unaona, hivyo ndivyo yalivyo hafifu. Mtu angewezaje kuwa hivyo? Huo ni weusi na giza, tofauti za kimadhehebu zikiwakatilia mbali na baraka za Mungu. Hilo liko katika madhehebu yote. Hiyo ni kweli. Ndugu, usimwendee *mke*, nenda kwa Mume. Usichukue jina la *mke*; chukua la Mume, unaona, chukua Jina la Mume.

247 Unasema, “Ndugu Branham, utalifanya hilo litie nanga vipi leo? Utafanyaje jambo hilo?”

248 Alitoa ahadi ya kwamba Yeye angelifanya hivyo, kasema, “Msiogope, enyi kundi dogo, kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule Ufalme.”

“Atafanyaje jambo hilo?”

249 Yeye angali ni Yehova-Yire. Yeye angali ni Yehova-Yire. Mungu anaweza kujipatia Kanisa. “Yeye anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Yeye, hakika, Yeye ni Yehova-Yire.

Unasema, “Je! itafanikiwa?” Ni hakika. Mungu aliliahidi.

“Je! unafikiri utawahi kufaulu . . .?”

250 Siwezi, lakini Yeye atafaulu. Mimi siwajibiki kwa kulifanya lifaulu. Ninawajibika tu kwa kulihubiri. Ni kazi Yake kulithibitisha. Ni Yeye. Kama nikisimama na Kweli, Yeye ataitetea. Kaishalithibitisha, naye atalitenda.

Unasema, “Kuna giza nene sana.”

251 Naam, ninajua kuna giza nene sana. Na makanisa yote yanaingia kwenye shirika hili kubwa mno, kwenda machinjioni.

“Kwa hiyo utafanyaje juu ya jambo hilo?”

252 Inanikumbusha tu juu ya hadithi moja ndogo. Huenda niliseme jambo hili kabla tu ya kufunga. Huko Carlsbad, New Mexico, hapa, wana mapango kule, mwajua. Ina—inawabidi washuke chini kama maili moja, chini kwenye hayo. Kamwe sikupenda kitu hicho. Daima wako kama fuko ardhini. Na ukishuka kule chini, na, loo, inakuwa giza la usiku wa manane chini kule. Na kuna maskini msichana huyu mdogo anayesimama, loo, labda, kama kile kitu kidogo *pale*. Na maskini ndugu yake mdogo alikuwa amesimama *hapa*, upande mmoja, pamoja na kiongozi aliyekuwa akiwapeleka huko chini. Kwa hiyo walikuwa wamesimama huko chini mahali hapo penye giza, na kulikuwa na nuru wakati huo, walikuwa wamewasha taa zote. Na mtu huyu, kwa kuninii tu. . .

253 Huyu kiongozi alichurupuka akaenda kwenye taa. Na mvulana huyu mdogo alikuwa akitembea pamoja naye, akimwangalia huyo kiongozi. Kwa hiyo huyo kiongozi alifika *pale*, akashika swichi hii na kuizima tu hiyo swichi. Loo, jamani, nena kuhusu giza! Maili moja ndani kabisa ya ardhi, unajua, giza sana hata usingeweza kutikisa mkono wako, usingeweza kuona chochote.

254 Naye maskini msichana huyo alikuwa akipiga kelele kwa nguvu zake zote. Alikuwa tu akiruka-ruka na kupiga kelele, akipiga kelele kwa nguvu kadiri alivyo- . . .

255 Na kutokana na kelele hizo zote, mvulana huyo mdogo akiwa amesimama upande mmoja, alisema, “Loo, maskini dada! Loo, maskini dada!”

Akasema, “Unataka nini, ndugu mdogo?”

256 Kasema, “Usiogope. Yupo mtu hapa anayeweza kuziwasha taa.”

257 Yupo mtu hapa anayeweza kuziwasha Taa. Yeye, Yeye ni Yehova-Yire. Unaona? Yupo Mtu hapa, aliye miongoni mwetu usiku wa leo, Roho Mtakatifu, Yeye anaweza kuziwasha Taa. Yeye ni Neno, Mtu aliyepo hapa anayeweza kuziwasha Taa. Sijui jinsi atakavyoziwasha. Si kazi yangu kujua, bali Yeye anajua jinsi ya kuwasha swichi. Aliweka ahadi. Aliweka kule juu wakati Ibrahimu alipokuwa ameinua kisu chake juu ya shingo ya mwanawe; akaiwasha Taa. Naam. Yeye anaweza kuiwasha Taa tena usiku wa leo.

258 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Mungu na asaidie, ya kwamba ataiwasha hiyo swichi ndogo moyoni mwako.

259 Wapendwa, juma hili mmemwona Roho Mtakatifu mkuu miongoni mwetu. Hakuna swali kuhusu hilo. Lakini, loo, hebu Taa hiyo ndogo na iwashwe, usiku wa leo. Usikose Hilo, ndugu yangu, dada. Nafikiri ya kwamba kwa mlango huu mmoja tu mfupi hapa wa—wa Ibrahimu, umethibitisha, tukiushikamanisha tu huku na huku, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, umethibitisha tunaishi kwenye majira gani; Kristo, akiwa amekataliwa katika taifa letu tena; matetemeko ya nchi mahali mahali; Sodoma na Gomora; kanisa katika hali yake, likifanya sanamu ya mnyama hasa. Mambo haya yote yametukia, kama vile Biblia ilivyosema, na ninyi watu mnajua jambo hilo. Unaona? Sasa bila ya tukio hili kuu pamoja na Kristo, kama Uzima wa Kristo ukija ndani yako . . .

260 Sasa hebu jiangalie tu katika kioo cha Mungu, na uone tu kama unaweza kujitambulisha usiku wa leo. Kama ungelikuwa ukiishi katika siku za—za Nuhu, katika wakati wa ile gharika, ungetambulishwa na upande gani? Kama ungelishi katika siku za Musa, ungelikuwa upande gani? Kama ungelishi katika siku za Kristo, wakati makanisa yote yalipokuwa yakimpinga? Ilimbidi kusimama peke yake huko nje, na mambo aliyofanya. Jambo pekee, Mungu alikuwa pamoja Naye, hilo ndilo jambo pekee. Hata wanafunzi Wake wote, karibu wote, walimwacha. Lakini ni upande gani, hali tu uliyo nayo sasa, ungeninii wapi, utakuwa uko upande gani? Ungekuwa upande gani sasa hivi, wakati unapomwona tena papa hapa miongoni mwetu?

261 Sasa Yeye yupo hapa, Naye anaweza kuiwasha Taa moyoni mwako, na kuyajaza tu maisha yako kwa Roho Mtakatifu. Ni wangapi waliomo humu ndani sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na mioyo yenu, pia, watakaomba pamoja nami kwa dakika?

262 Sasa, Baba wa Mbinguni, tunajua ya kwamba Wewe huji tu na—na kufanya mambo kusudi tu uonyeshe ya kwamba unaweza kuyafanya. Unayafanya kwa kusudi fulani. Na, Bwana, juma hili, nilijisikia kuongozwa kungojea mpaka dakika hii, wakati uu huu, ili kwanza waweze kuona ya kwamba Neno hilo limethibitishwa. Hakuna swali tena sasa. Na mtu huyu mmoja, Ibrahimu, wakati watu wote katika Biblia wamefungashwa moja kwa moja kwenye jambo hilo, nasi tunaona mahali tunapoketi sasa hivi.

263 Baba, nikiwa na neno lililovunjika-vunjika, bali hivyo ndivyo vizuri kabisa ningaliweza kufanya. Ninaomba sasa ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu aliyepo hapa, anayejua siri za kila moyo, atasema na moyo huo sasa hivi. Lijalie, Bwana. Sema na yule ambaye asingeenda, kama ulikuwa ukija usiku wa

leo, kama mlango ungefungwa usiku wa leo, kama wangekufa wakienda zao nyumbani, ama wagongwe na gari na kuuawa, ama wafe, wakutwe wamefia kitandani asubuhi, wasingeokoka. Ee Mungu, tafadhali usiache hata mmoja wao apitie njia hiyo.

²⁶⁴ Kama wamejiunga tu na kanisa, Bwana, jalia wasione haya kujitokeza na kumwomba Mungu awajaze na Roho Wake, ili Uhai Wake upate kuingia ndani yao. Kama hawajaweza kufahamu mambo haya; wala wanafunzi hawakuyafahamu, bali walishikilia mpaka Roho Mtakatifu alipomwagwa, ndipo wakalifahamu Hilo, kisha wakaandika Biblia. Ninaomba, Baba, sasa, ya kwamba utasema na kila moyo na ujalie wajue ya kwamba Mtu anayeweza kuiwasha Taa yupo papo hapo kwenye mlango wa moyo wao.

²⁶⁵ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa. Ni wangapi humu ndani watakaokuwa waaminifu kabisa, na kusema, “Ndugu Branham, ni—ninajua ya kwamba siko sawa na Mungu”? Ninataka—ninataka uinue mkono wako juu. Endelea tu kuinamisha kichwa chako, kila mtu, ila uinue mkono wako. “Mimi siko sawa mambo yangu na Mungu.” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Naam. “Mimi,” mikono, “ninajua siko sawa mambo yangu na Mungu.”

²⁶⁶ Unaona, kile ninachojaribu kufanya, kupata kibali cha Mungu kwa ajili ya ibada hii kuu ya uponyaji kesho. Kama ninaweza tu kupata kibali, si—si—siamini kutakuwa na kitu kitakachosalia ila kile ambacho, Mungu ataponya, endapo tu ninaweza kuwafanya watu waamini.

²⁶⁷ Sasa, ninyi msio na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na mnajua hayo ndiyo Mafuta. Kama hukuwa na Mafuta kwenye taa, hawakuingia.

²⁶⁸ Nanyi je! mlipata kusikia juu ya wakati kama huo, kwenye magazeti, ambapo Wapresbiteri, Walutheri... Angalia kwenye gazeti la Wafanyabiashara Wakristo. Walutheri, Wapresbiteri, hata Katoliki, wanatafuta kupata ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa mamia. Nami sijui kama hao Wafanyabiashara Wakristo wanafahamu ya kwamba hawatampata?

²⁶⁹ Biblia ilisema, “Walipokuja, kasema, ‘Tupeni mafuta yenu kidogo,’ wakasema.” Wanawali waliolala, walitambua ya kwamba walikuwa na wakati huo wote wa kupata Mafuta, bali hawakuyapata. Kwa hiyo wakati Bwana Arusi alipokuwa karibu sana na kuja, wao walisema, “Tupeni Mafuta yenu kidogo.” Wakasema, “Tuna ya kututosha tu sisi wenyewe. Afadhali shikeni njia mwende mkanunue kwa hao wauzao.” Ndipo walipokuwa wameondoka, Bwana Arusi akaja, naye Bibi-arusi akaingia. Nao wakatupwa katika giza la nje, kuamka na kukuta Unyakuo umekwisha kutukia. “Nao wakaachwa ambako kutakuwa na kilio na kuomboleza,” wakati wa ile Dhiki, “na kusaga meno.”

270 Ndugu yangu, dada, usiku wa leo, rafiki yangu, kama huna Roho Mtakatifu, je! uta...ama umeshawishika vya kutosha kujua ya kwamba unapaswa kumpata, je! waweza kuinua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham. Ninaamini tuko Mbele za Mungu. Niombee. Mimi sina Roho Mtakatifu.” Mungu akubariki. Angalia tu mikono hiyo, kila mahali. Je? unamtaka, basi?

271 Sasa ninajua, kwenu ninyi Wamethodisti na Wabaptisti, na kadhalika, kuna ulokole mwingi sana unaofuata ujumbe wowote.

272 Sasa kwenu ninyi Walutheri. Nilikuwa tu nikisoma historia ya Martin Luther hivi punde, kimoja cha vitabu vilivyoandikwa juu yake, hapa si muda mrefu uliopita. Walisema, “Halikuwa ni jambo la ajabu sana kwamba Martin Luther angeweza kulipinga kanisa Katoliki na kuepuka, lakini ni kule kusimama wima dhidi ya ulokole wote ulioufuata ufufuo wake.”

273 Na hilo linaambatana, kuna umati uliochangamana mno katika kila ufufuo. Mnajua jambo hilo. Lakini sasa, kumbukeni, hilo linaonyesha tu ya kwamba kuna ulio halisi. Unapooni dola ya bandia, ama mtu fulani anajifanya kana kwamba wana kitu fulani, kumbuka tu kuna kimoja kilicho halisi ambacho kimeigizwa. Kama siyo, hicho ndicho cha asili. Unaona? Kwa hiyo unajua ya kwamba hicho hakiwezi kuwa cha asili, kwa hiyo hapana budi kuwe na cha asili.

274 Na hicho cha asili ndicho Yesu Kristo halisi, Yule aliyepo hapa, ambaye anajua kila siri ndani ya moyo wako sasa hivi. Na sasa nitawaulizeni, kama mmemwona, na kusikia shuhuda hizi za kila namna ya vitu viponywa, na jinsi ambavyo mioyo ya watu imefunuliwa kote katika juma hili, nanyi... Huyo ni Yeye akinena nawe. Huyo ni Yeye. Sijui kama ungeamini ya kwamba mimi nikiomba, na kwa ajili yako, ingekusaidia?

275 Kumbukeni, Roho Mtakatifu alitolewa kwa kuwekewa mikono. Petro, baada ya Filipo kushuka kwenda Samaria na kuwabatiza watu wote kule, katika Jina la Yesu Kristo, bado, Petro alishuka akaja akawawekea mikono, ndipo Roho Mtakatifu akawashukia. Unaona?

276 Sasa kama unaamini jambo hilo, sijui kama ungekuja hapa, kila mmoja ambaye hajaokoka, ama asiye na Roho Mtakatifu, atakuja hapa na kusimama papa hapa kwa dakika moja tu, nikuombee. Kama ukija tu kutoka kwenye marefu ya kanisa, haidhuru uko wapi, simama tu hapa. Njoo huku tu na hebu mimi—hebu niombe pamoja nawe dakika moja. Mungu awabariki.

277 Sasa hebu tu kila mtu aimbe sasa. *Karibu Nishawishike*, mkiweza. Dada Downing, hapa, tafadhali. Vema.

278 Hivi hamtakuja moja kwa moja *hapa*, ndugu zangu? Mungu akubariki, ndugu yangu. Kila mtu atulie kabisa sasa,

akiomba. Huenda huu ukawa ndio wakati muhimu sana, huenda ukamaanisha tofauti kati ya mauti na Uzima, kwa watu wengi, wengi sana.

279 Je! nyote mmekuwapo hapa juma hili? Je! mmemwona Roho Mtakatifu, yale aliyofanya juma hili miongoni mwa watu?

“... wishike,” kumpokea Kristo;

Loo, Yeye sasa, nafsi fulani kuninii. . .

280 Hivi si uje, ukiwa huna Mungu, huna Roho Mtakatifu? Je! unasema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa, Ndugu Branham”? Hilo ndilo, silo ninalozungumzia. Ninamaanisha, je! umejazwa na Roho wa Mungu?

“... zaidi. . .”

281 Kamwe hutapata siku yenye nafasi zaidi kuliko sasa hivi, wakati Yesu Kristo ametambulishwa miongoni mwetu.

“... Kwako. . .”

282 Vipi kama ungekufa kabla ya asubuhi? Na halafu huwezi kupiga simu. Hivi huwezi kuja sasa wakati Yeye anaita?

“Karibu nimeshawishika,” . . .

Hiyo ni kweli, endeleeni kushuka kuja moja kwa moja huku.

. . . njoo, njoo leo;

“Karibu nimeshawishika,” usigeuke. . .

283 Je! hutapenda kuja sasa? Ninajua kitu fulani moyoni mwangu kinaniambia ya kwamba kuna mtu fulani anasitasita. Usifanye hivyo, ndugu, usifanye hivyo!

. . . Malaika wamekaa karibu,

Maombi yanatoka kwenye mioyo ya thamani sana; Ewe mwenye kutangatanga, njoo. (Sasa kwa ninii sana. . .)

284 Sikiliza, rafiki. Unaamini ya kwamba Roho Mtakatifu, kote katika juma hili, amethibitisha ya kwamba Yeye hunena hapa? Hebu tuone mkono wako. Kunapaswa kuwe na watu wengi zaidi ya hawa, ama zaidi. Ninahisi Hisi hiyo. Unaona, Yeye si ninii. . . Kuna kasoro fulani bado. Afadhali mje.

285 Kumbukeni, siwezi—siwezi kuwalazimisha mje kama hamtaki. Lakini ninaamini huenda huu ukawa ndio wakati wenyewe, yote hayo uliyotazamia, huenda yakawa karibu kutimia sasa. Na huu huenda ukawa, natumaini sivyo, huenda ikawa ndio wakati wa mwisho utakapopata kuitwa. Kumbuka, Yeye hatashindana daima. Ataita, kisha atakuacha, asiye tena kamwe.

286 Mbona usije sasa hivi? Hivi huwezi kuja hapa na kujiwakilisha tu mwenyewe mbele za Mungu? Useme, “Nitakuja nisimame. Nitafuata njia hiyo. Mimi sioni haya. Mimi ni mfuasi wa kanisa, bali ninataka ulimwengu wote ujue ya kwamba

niko tayari kumpokea Kristo moyoni mwangu, Roho Mtakatifu. Ninakuja sasa kufanya hivyo. Niko tayari kunyosha mambo, niwe Mkristo halisi, bibi halisi, mwanamume halisi.” Hivi si uje? Tutangojea tu. Njoni moja kwa moja huku, hiyo ni kweli, kutoka kwenye hizo roshani na marefu ya kanisa. Shukeni mje hapa, mchukue tu msimamo wenu.

²⁸⁷ Rafiki, huenda nisikuone tena upande huu wa wakati huu mkuu. Lakini kama nisipokuona, kumbuka, nitakuwa sina hatia sasa, na Kristo pia. Yeye amejitambulisha Mwenyewe pamoja nawe. Utamwona akifanya jambo lile lile hivi punde. Vema. Sasa shukeni mje, mchukue msimamo wenu.

²⁸⁸ “Mbona,” unasema, “Ndugu Branham, unanihukumu.” La, sikuhukumu.

²⁸⁹ Ninahukumu Hisi hii iliyo ndani yangu, unaona. Kuna kitu fulani humu ndani, kinachosema, “Loo, kuna wengine zaidi. Kuna wengine wengi.” Mnaona?

²⁹⁰ Sasa unasema, “Vema, mimi, nimejiunga na kanisa, Ndugu Branham. Mimi ni Mpentekoste. Si—si—sininii...” Sisemi jambo hilo, ewe rafiki. Siulizii hilo, hata kidogo.

Ninauliza, “Je! wewe una Uzima wa Kristo?”

²⁹¹ Nawe unasema, “Ndugu Branham, nilinena kwa lugha.” Hilo ni jambo zuri. Lakini hilo bado silo ninalonena habari zake.

²⁹² Unasema, “Ndugu Branham, sijapata kumdhuru mtu yeyote.” Hilo bado silo ninaloulizia.

“Je! Uzima wa Kristo umo ndani yako?”

²⁹³ Usibahatishe, rafiki. Kamwe, kamwe, kamwe usifanye hivyo. Itakuwa ni wakati utakaponinii... Wakati mauti yatakapokupiga, umechelewa sana wakati huo. Usifanye hivyo. Tafadhali usifanye hivyo.

²⁹⁴ Sasa tuna wengi sana hapa hivi sasa, itanibidi kutoa nafasi zaidi kwa wengine zaidi. Nitawaombea hawa, na halafu ili tupate kuingia, tuingie kwenye chumba mle ili tuje tuwawekee mikono, wampokee Roho Mtakatifu. Na halafu tutaomba sasa hivi kwa ajili ya hawa.

Inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja.

²⁹⁵ Baba yetu wa Mbinguni, hapa kuna wale walioinamisha vichwa vyao hapa, ambao ni wanaume na wanawake, ni watu wanaoelekea kwenye Umilele. Wao, hawana budi kwenda, tunajua jambo hilo. Nasi tunaona matetemeko ya nchi, ambapo, na ulimwengu katika hali uliomo sasa. Na tunaona Kristo akija kwetu na kufanya mambo anayofanya, na kuuona Ujumbe, Neno likitoka moja kwa moja, na kisha kumwona Yeye akija moja kwa moja nyuma Yake na kulithibitisha kwamba ni Kweli, akijua kila siri ya moyo. Na watu hawa sasa wamekuja mbele

kuchukua msimamo. Wasingeweza kufanya jambo hili wao wenyewe. Wamekuja kwa sababu waliongozwa kuja.

²⁹⁶ Na, Baba, ninawaombea papa hapa. Si kwa ajili tu ya wokovu wao, kuokolewa, bali wapate kujazwa na Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Jalia kila mmoja anayesimama hapa ajazwe na Roho, na jalia kutoka hapa uje ufufuo kote katika nchi hii, ambao utatikisa jumuia hii na maeneo haya yote yanayoizunguka. Tujalie, Bwana.

²⁹⁷ Na kila kanisa, na Methodisti, Baptisti, Presbiteri, kanisa la Kristo, Lutheri, lolote lile, jalia uje ufufuo, Bwana, wa watu hawa kurudi na Roho Mtakatifu halisi akimdhihirisha Mungu maishani mwao. Tujalie, Baba. Hao ni Wako sasa, nami ninawakabidhi Kwako. Sasa tutawaingiza ndani na kuwawekea mikono, Bwana, kusudi wampokee Roho Mtakatifu. Katika Jina la Yesu.

Sasa wakati sisi sote tumeinamisha vichwa vyetu chini.

²⁹⁸ Ninaliomba kundi *hili* sasa, mfuateni mtu *huyu* papa hapa karibu na wewe, kwamba aninii, tuwapate huku nyuma chumbani. Tuna mahali hapa kwa ajili yenu kupiga magoti; tuje tuwawekee mikono, mpate kumpokea Roho Mtakatifu. Na kama ukiwa mgonjwa, utaponywa. Na chochote unachohitaji, nenda moja kwa moja hapa sasa. Tunaweza kuingia moja kwa moja pamoja nanyi. Kuna wengine wanaopaswa kuja, bali wao—wao kidogo ni... Hakuna nafasi kwao ya kusimama. Tunataka tu kuufanya huu ukumbi maradufu; sawa, ingieni moja kwa moja humu, huku—upande huu *hapa*. Hilo ni sawa. Mungu awabariki.

²⁹⁹ Sasa, kwa wengine wenu hapa sasa; wanapotoka, mbona msije moja kwa moja hapa tena sasa, kwa ajili ya maombi. Na tupajaze mahali hapa tena, hapa karibu sasa.

³⁰⁰ Tunaingia mle kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunaingia.

³⁰¹ Baada ya sisi kuona utambulisho wa huyo Bwana Yesu hapa mbele zetu, juma hili, na kujua bila shaka yoyote, ya kwamba huyo ni Yeye hapa. Sasa kumbukeni, Roho Mtakatifu yule yule, Yesu yule yule ambaye angeniambia shida ya watu hao ilikuwa ni nini, kwamba walikuwa wapi, kwamba wao ni akina nani, mahali walipotoka, kile kitakachowapata. Nanyi mnajua halijakosea hata wakati mmoja; wala halitashindwa, halitashindwa kamwe. Roho Mtakatifu yeye huyo aliniambia nifanye jambo hili. Hiyo ni kweli. Ninalifanya kwa uongozi wa Roho Mtakatifu.

³⁰² Sasa wakati hili, mara kundi hili likitoka kwenye chumba hiki kingine hapa, kabla hatujaenda kule, tunawataka mje sasa. Ninyi hapa, njoni, sogeeni upande huu sasa. Wengine wenu hapa wanaotaka ubatizo wa Roho, mbona msije sasa hivi. Sogeeni huku. Mungu akubariki, kijana mwanamume. Na endapo wengine wenu ni wagonjwa, na hamjajazwa na Roho

Mtakatifu, kwa nini msije mkampokee Kristo, mumpokee na ndipo mtakuwa na hali nzuri zaidi usiku wa leo.

³⁰³ Mama huyu alikuwa tu amepatwa na ninii... ameshawishika sana kana kwamba asingeweza kuvumilia jambo hilo. Wanamsaidia kumpeleka kwenye chumba. Njoni sasa, ninyi, ninyi wengine sasa. Kuna nafasi tele ya kusimama hapa sasa. Njoni huku, ninyi ambao ni wafuasi wa kanisa, Wamethodisti, Wabaptisti. Hatuwaombi kuninii...

³⁰⁴ Sikilizeni, enyi marafiki, ninajua wanasema, "Pentekoste, walifanya pentekoste kuwa dhehebu." Hilo ni kosa.

³⁰⁵ Pentekoste ni tukio. Wamethodisti wanalipata. Wabaptisti wanalipata. Wote wanalipata. Pentekoste si dhehebu. Ni tukio. Na kama hujapata tukio la pentekoste, njoo ulipokee sasa. Kumbuka, kama unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, nabii Wake, kumbuka, kuna ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu. Moja kwa moja katikati ya ulokole wote, kungali kuna Roho Mtakatifu halisi, Uzima halisi. Njoni, aminini Hilo sasa hivi.

³⁰⁶ Hivi hamwezi kuja wakati tukiimba aya moja tu, mbili zaidi za wimbo huu, ili kwamba niweze kuwa na hakika ya kwamba nafsi yangu ni safi nitakapoondoka katika mji huu sasa, hiyo damu haitakuwa juu yake? Ninajua Yeye anazungumza na wengine. Mbona msije?

"...wishika" sasa ku-...leo;

Mungu akubariki, mvulana mdogo. Mungu awabariki ninyi nyote mnaosimama hapa sasa.

"Ka..." (Hiyo ni kweli. Njoni.) "...-ribu nimeshawishika,"

³⁰⁷ Njoni huku, kutoka upande wowote wa jengo. Nje, ndani, roshani, popote pale, shukeni mje moja kwa moja huku sasa, moja kwa moja huku. Mteteeni Kristo. Msimwonee aibu. Kama ulikuwa ukifa; vipi kama ulisikia moyo wako ukirukaruka sasa hivi? Na, kumbuka, Huyo anayesema nawe, Yeye anaushikilia moyo wako mkononi Mwake. Anajua siri ya moyo wako. Ninasema jambo hilo katika Jina la Bwana, kuna wengi zaidi hapa wanaopaswa kuja. Mbona usije? Unasema, "Je! ni mimi, Ndugu Branham?" Naam, ni wewe. Kama huna hakika, usibahatishe.

...ya thamani sana; Ewe mwenye kutangatanga, njoo.

"Karibu nimesha-..." (Namna hiyo. Namna hiyo.) "...-wishika," mavuno...

Hiyo ni kweli, mavuno karibu yamekwisha. Njoni.

"Karibu..."

³⁰⁸ Siku moja, itakuwa mtu umechelewa sana. Usingojee saa nyingine, dakika nyingine. Amka mara moja na uje huku.

Ewe kijana mwanamume, mlete mpenzi wako msichana. Mlete mpenzi wako mvulana. Mama, mlete baba. Njoni, sasa hivi, kila mtu. Kijana mwanamke, kijana mwanamume, yeyote yule uwaye, mzee, bibi kizee, njoni. Namna hiyo. Kama wewe ni mkongwe, kumbuka yale niliyowaonyesha sasa hivi, kwa Biblia, utabadilishwa kama tu utaukubali Uzao wa Ibrahimu.

...yote yatashindwa!

Huzuni, huzuni, kilio hicho cha uchungu:

“Karibu sana, bali umepotea!”

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

³⁰⁹ Bwana Yesu, Ee Mungu, uchunguze kila moyo. Chunguza kila mtu, Ee Roho Mtakatifu Mkuu. Ee Mungu, jalia lisiwe bure kwa huyu, hata mtu mmoja. Jalia kila mmoja, kila mmoja, Bwana, aokoake. Usimruhusu hata mmoja wao apotee, Bwana. Ninawadai, katika Jina la Bwana Yesu, kwa ajili ya—kwa ajili ya vito vya taji ya Bwana wangu, loo, ambaye Uwepo Wake upo hapa sasa, ile Nguzo kuu ya Moto ikisogea humu jengoni, ikipitia kwenye mioyo. Ninaomba, Mungu, ya kwamba moyo huo utavunjilia mbali pingu hizo, na kuamka na kuja kwa utamu kwa Yesu Kristo, useme, “Bwana, yote niliyo, mimi hapa. Nichukue na unifinyange, Bwana, katika nyumba Yako kuu ya kufinyanga; na unijaze, na unifanye mwana ama binti wa Mungu.” Nijalie, Bwana. Jalia hili liwe hivyo.

³¹⁰ Tunapoendelea kuimba aya moja zaidi, je! mtakuja? Ndipo itatubidi kufunga sasa, upesi, maana inatubidi kuja hapa pamoja na hao wengine.

“Karibu nimeshawi-...”

³¹¹ Njoni sasa. Njoni sasa hivi, sivyo? Mungu akubariki, mpenzi. “Katika vinywa vya watoto wachanga, Yeye anapokea sifa.”

Loo, “Karibu nimeshawishika,” loo, usirudi;

Yesu...

³¹² Huyu ni Yeye akikualika, akinena na moyo wako. “Sijui kama ni mimi?” Kama kuna chembe moja ya tashwishi, njoo!

...wanakaa karibu,

Maombi yanaibuka kutoka kwenye mioyo ya thamani sana; Ee mwenye kutangatanga, njoo.

³¹³ Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, wakati hawa wanapojitayarisha. Sasa mnaposimama hapa, hebu angalieni tu chini. Unakumbuka, ilikubidi kuja kwa kusema...mdundo wa kitu Fulani ndani yako, ukikwambia kuna kasoro fulani ndogo maishani mwako. Ninapendezewa na msimamo wako. Kumbukeni, Yesu alisema, “Mkinionea aibu mbele za watu, nitawaonea aibu mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Lakini yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

³¹⁴ Na sasa kuna watu kadhaa hapa huko nyuma sasa, walio tayari kujiunga nasi sasa katika maombi, mpate kuokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu. Mwambie tu unasikitika kwa yale uliyofanya, nawe utakuwa Mkristo tangu sasa na kuendelea, kwa neema Yake, na unataka ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao utakuongoza katika safari ya maisha.

³¹⁵ Baba wa Mbinguni, hao ni johari katika taji Yako. Wasingaliweza kuja, wasingaliweza kuja, pasipo kuonywa na kitu Fulani. Nawe ulisema, “Hakuna mtu anayeweza kuja asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja.” Nao hawa hapa wanakuja, kwa kitu Fulani kikiwaambia waje. Ndipo unaanza kazi fulani, Bwana. Ninaomba ya kwamba utaimaliza, usiku wa leo, ndani yao, Bwana, kwa kuwafanya wana na binti za Mungu. Tujalie. Jalia hata mmoja wao asipotee. Ninawakabidhi Kwako sasa kama tuzo la Neno Lako na Uwepo Wako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³¹⁶ Sasa rudini moja kwa moja kwenye kile chumba, mpaka tutakapoweza kuwafikia. Elekeeni kulia, hapa. Mabawabu watawaongoza wawarudishe moja kwa moja.

³¹⁷ Na sasa—sasa sijui kama wasaidizi wote wa kibinafsi watakuja, wawafuate hawa moja kwa moja ndani, wengi wa wasaidizi wa kibinafsi kutoka kwenye makanisa mengine.

³¹⁸ Ninyi wahudumu mnaotaka kurudi kule ndani pamoja na sisi sasa, kuona kama jambo hili limefanywa vizuri ama halijafanywa vizuri, njoni, rudini pamoja nasi. Njoni, pigeni magoti pamoja na watu wenu, kusudi wampokee Roho Mtakatifu. Kila mmoja, njoo moja kwa moja na... Ninyi wahudumu, yeyote wenu, Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, haidhuru wewe ni nani, njoo huku. Unaalikwa. Njoni pamoja na watu hawa.

³¹⁹ Nanyi wasaidizi wa kibinafsi kutoka makanisa mbalimbali, mnaojua jinsi ya kuomba pamoja na watu, wawekeeni mikono, njoni sasa. Hawa ha—hapo wamewekwa mikononi mwenu; wao ni tuzo la Neno. Hivi hamwezi kuja sasa wakati huu, wasaidizi wenu wa kibinafsi, kisha mrudi huko nyuma, kabla hatujaubadilisha mkutano hapa kwa dakika moja tu. Njoni sasa, ingieni moja kwa moja. Hilo ni sawa. Rudini moja kwa moja humo kwenye hicho chumba, nafasi tele huko nyuma sasa. Rudini moja kwa moja nyuma na mfanye kila mwezacho kuwasaidia watu hawa wapenzi. Hapo, Yesu amewaleta; Yeye amewashika kwenye wavu wa Injili. Sasa ninyi warudisheni kule na hebu tuombe pamoja nao, kwamba Mungu atamjaza kila mmoja wao na Roho Mtakatifu. Fungeni milango, kaeni mumo humo mpaka itendeke. Aliahidi itatendeka. Naye aliahidi hilo, na atatimiza ahadi Yake. Yeye ni mwaminifu vivyo hivyo tu kwa ahadi Yake, kama kutokea mbele yetu.

Bwana, wabariki!

³²⁰ Wahudumu, je! mpo hapa? Wahubiri, walei, wanaopenda kuangalia ama kuwafanya watu wampokee Roho Mtakatifu, ni mahali penu pa kazi sasa, nendeni pamoja nao, simameni karibu na watu wenu, ninyi watu mliofunzwa vizuri mlio na ujuzi wa Roho Mtakatifu; na ninyi akina mama mliofunzwa vizuri mnaojua maana yake, nendeni kwa wale dada huko nyuma mahali walipo. Ninyi mnaojua la kufanya, kaeni pamoja nao huko nyuma sasa. Sasa hivi ndio wakati wenu. Huu ndio wakati wa jukumu lenu. Hii ndiyo rangi yenu, nendeni sasa. Mungu awabariki. Hiyo ni kweli. Simameni kwenye nafasi zenu tu na mwingie moja kwa moja pamoja nao pale, na mkae pale na mhakikishe ya kwamba—ya kwamba imetendeka, na imetendeka ipaswavyo. Kaeni humo mpaka mtakapooni utamu wa Kristo ndani ya kila mmoja wao. Mungu atakuheshimu kwa ajili ya jambo hilo. Amina, na amina.

Loo, napenda hilo. Angalieni tu kile kilichorudi kule nyuma!

³²¹ Je! yupo mmoja zaidi humu ndani ambaye hakuingia, ambaye anapaswa kuingia? Kama yupo, utaamka na uwafuate hawa wasaidizi wa kibinafsi uingie moja kwa moja? Fanya hivyo, je! utafanya hivyo? Kama kuna mmoja humu ndani ambaye—ambaye hajisikii hivyo—ya kwamba uko tu pale unapopaswa kuwa.

³²² Sasa, kumbuka, ndugu, dada, si—siwezi kufanya jambo hili litukie. Unaona, Mungu Ndiye anayefanya mambo haya, si mimi. Sasa ninaomba ya kwamba Mungu atawajalia mambo haya, na kuwapa tu—tu—tukio la ubatizo wa Roho Mtakatifu.

³²³ Ninyi watu wote sasa mnaompenda Bwana Yesu, na mnataka kuingia na kuomba, rudini huku nyuma sasa na mkaombe pamoja na watu hawa. Je! mtafanya hivyo? Asanteni. Asanteni, sana.

³²⁴ Mwajua, ninapowaona wasaidizi wa kibinafsi wakienda pamoja na watu, ninaninii...ninataka kusema jambo hili kuwahusu ninyi watu hapa, hilo linathibitisha kile mlichio. Nimeenda sehemu nyingi, hata, na watu wanaodhaniwa kuwa wamejazwa na Roho, nao wanaona miito ya madhabahuni ikitolewa, na, mbona, usingeweza kuwafanya watu hao waingie pamoja na mtu yeyote, kuomba pamoja nao. Unaona, hiyo inaonyesha ya kwamba ni *Ikabod*, “Roho wa Bwana ameondoka.” Mnaona? Lakini wakati unapooni hizo juhudi na Moto na shauku, na kuzionea shauku nafsi za wanadamu!

³²⁵ Mnaona, juma hili lote, nimechukua tu wakati wangu, na kuangalia utambuzi na mambo kama hayo, ili kwamba watu walipate na wajue Roho Mtakatifu yuko karibu, kisha nitoe wito huo wa madhabahuni. Ninyi wahudumu mnafahamu nililokuwa nikifanya? Mnaona, kufanya wito wa madhabahuni sasa wakati wao walikuwa wameshawishika, sasa mamia yao wamo mle

ndani sasa kumpokea Roho Mtakatifu. Na wengi waliingia pamoja nao, kuomba pamoja nao.

Sasa kama kuna mtu mwingine yeyote hapa, ili kwamba . . .

³²⁶ Nitasema jambo hili, ya kwamba mmeona Uwepo wa Kristo, juma hili, akijitambulisha Mwenyewe hapa. Mmemwona.

³²⁷ Na sasa kumbukeni, ya kwamba, hakuna damu itakayokuwa juu yangu Siku hiyo, kama ni kesho. Itakuwa, moja ya siku hizi. Kumbukeni tu, tutaenda kusimama Pale. Haidhuru wewe ni nani, utaenda kusimama Pale, hata hivyo. “Imeamriwa mtu kufa mara moja, na baadaye Hukumu,” nasi tutaenda kusimama Pale.

³²⁸ Sasa kama wewe huna uhakika kabisa ya kwamba una Kristo, Roho Mtakatifu moyoni mwako, Naye anajithibitisha Mwenyewe mle ndani, kwa upendo na amani na furaha na matunda ya Roho, na Uhai wa Kristo ukiishi ndani yako, basi, kumbuka, damu yako haimo mikononi mwangu. Wala Yeye hatakuwa na hatia, maana ameonekana mbele yenu, na kujionyesha hapa kulingana na Maandiko kabisa. Ni wangapi watashuhudia jambo hilo, kwa kuinua mkono wako, useme, “Nimeona jambo Hilo juma hili”? Hiyo ni kweli, unaona, basi hatuna hatia. Hatuna udhuru.

³²⁹ Sasa je! kuna yeyote anayetaka, mmoja zadi ambaye angetaka kuja? Ili kwamba niweze kusema, hapo wakati wangu utakapofika wa kuondoka hapa kesho, Bwana akipenda, ninaweza kusema, “Niko huru na damu yote kutoka kwenye ufufuo huo. Nilifanya vizuri nilivyoweza, Bwana. Ninalikabidhi Kwako. Sasa Wewe ninii tu. . . kila mmoja.”

³³⁰ Sasa ni wangapi humu ndani, ambao ni wagonjwa na ni wahitaji sasa, na wangetaka kuombewa, hebu tuwaone mkiinua mikono yenu. Vema, kote jengoni.

³³¹ Sasa nitawaomba mnifanyie jambo fulani. Sasa ninyi ni waaminio? Sasa ninataka mnifanyie jambo fulani sasa. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Wekeaneni mikono tu mmoja kwa mwingine, na sasa, angalieni, ninawatakeni muombe, ombeni tu.

³³² Sasa kumbukeni, watu wote watakaoingia kwenye mstari wa maombi kesho, wanapaswa kuwa hapa mapema, na wawe na kadi ya maombi. Ishike mkononi mwako itakapofikia wakati wa mstari sasa. Kama una mpenzi wako, ninyi ndugu wa Kimethodisti, Kibaptisti, Kipresbiteri, yeyote uwaye, kama mna wagonjwa, ambao, ninyi—ninyi njoni moja kwa moja nao, mje papa hapa mstarini nao. Njoo ujichukulie kadi ya maombi, maana . . . Kisha ulete kadi ya maombi moja kwa moja mstarini; mabawabu wataichukua. Watakuja na kuombewa.

³³³ Ninaamini Mungu atafanya mambo makubwa kesho. Ninatumaini atafanya. Hiyo ndiyo sababu ninafanya miito ya madhabahuni, ninafanya kila niwezalo, kupata kibali Kwake.

³³⁴ Sasa wakati sisi sote tunapoinamisha vichwa vyetu, na ninyi nyote mnaombeana. Sasa Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa wewe mwombee mwanamume ama mwanamke uliyemwekea mkono, kwa kuwa wao wanakuombea. Unaona? Usijiombee. Waombee. Wekeaneni mikono, na mwombe. Wekeaneni tu mikono. Hiyo ni kweli.

³³⁵ Sasa omba jinsi unavyoomba kanisani mwako. Useme, “Bwana Yesu, mponye maskini dada huyu, mpenzi; maskini ndugu huyu, mpenzi; yeyote yule awaye. Wao ni wagonjwa, Bwana. Nami—nami ni mwaminio, nami nitalifuata Neno Lako. Nalo Neno Lako lilisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.’ Nami ninaweka mikono yangu juu ya mgonjwa, mgonjwa huyu, ndugu huyu mgonjwa, dada huyu mgonjwa. Ni—ni—ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utathibitisha Neno Lako, na ishara itafuata, nao watapona.”

³³⁶ Bwana Yesu, ninawaombea, na kwa ajili ya lesa hizi; kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwamba utamponya kila mtu aliye katika Uwepo Wako wa Kiungu.

³³⁷ Shetani, umeshindwa vita. Wameuona Uwepo wa Kristo. Wamelisikia Neno Lake, wameliona likidhihirishwa. Wenye dhambi wamo mle ndani, wakitafuta wokovu. Umeshindwa vita. Ondoka ndani ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo. Waache, usiwatese tena.

³³⁸ Na jalia Mungu wa Mbinguni awafufue, wapate uzima tena, na afya nzuri na nguvu. Jalia hao walio na kadi za maombi hata isiwabidi kuja kwenye mstari wa maombi, kesho. Jalia Roho Mtakatifu alibubujikie kundi hili la watu, na amponye kila mmoja wao kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Sasa endelea, ndugu.



YEHova-YIRE ³ SWA64-0404

(Jehovah-Jireh ³)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 4 Aprili, 1964, kwenye Banda la Klabu cha 4-H huko Louisville, Mississippi, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org